IMANI katika MATENDO

Pigeni Tarumbeta katika Sayuni

** Ubatizo

** Kuumega Mkate

** Zaka

** Huduma katika Nyumba

** Piga mbiu ya Fundisho la Utume
Kuanzisha Vikundi vya Utume

** Kujenga Kanisa

"Wakawa wakidumu. . .
kila siku. . .
nyumba kwa nyumba"

Paul Galligan
HUDUMA YA UVUVIO AUSTRALIA

IMANI katika MATENDO

YALIYOMO

Huu muongozo umetolewa kwa ajili ya kujenga watakatifu, kuhusika kikamilifu katika kanisa la Maandiko Matakatifu, ambalo limo ndani ya nyumba. Linalowaleta pamoja mitume, makundi ya utume na makanisa katika eneo kufanya kazi ipasavyo, kutusaidia kuufikia utimilifu.

UTANGULIZI

SURA YA KWANZA: Tubuni Mkabatizwe
– Mfano wa Maandiko Matakatifu na tendo la Ubatizo

SURA YA PILI: Kuumega Mkate - Ibada isiyo ya Kidini
- **Kurejesha Meza ya Bwana kwa Watakatifu**
- **Kila siku, Nyumba kwa Nyumba**

SURA YA YATU: Zaka – Ufunuo wa Imani
- **Tunampa nani Zaka**
- **Kazi ya Zaka ni nini**
- **Tofauti kati ya Zaka na Sadaka**

SURA YA NNE: Kusudi na jinsi ya kuendesha Huduma katika Nyumba
-- Urejesho wa Kanisa katika Nyumba

SURA YA TANO: Piga Tarumbeta katika Sayuni
- **Pigia mbiu Fundisho la Mitume**
- **Kuanzisha Makundi ya Utume**

SURA YA SITA: Kujenga Kanisa
- **Kituo cha Shule ya Utume**
- **Kupanda makanisa mengi katika nyumba**

UTANGULIZI

Kulingana na Maandiko Matakatifu

Hatimaye, nyakati hizi Mungu ameanza kurejesha kanisa la Yesu Kristo**. Hili linafanyika Kulingana na Maandiko Matakatifu.** Wakati Bwana wetu alipokuja mara ya Kwanza na akathihirishwa katika Israeli, Maandiko mengi Matakatifu yaliyonenwa na manabii katika Agano la Kale yalitimia katika maisha, huduma na kufa Kwake. Mtume Mathayo kwa makini ananukuu katika Injili yake, Maandiko Mengi yaliyotimia kwa njia ya Yesu. **Huu ndio mfano. Neno la Mungu ndilo mamlaka ya pekee tuliyonayo kwa imani na matendo.** Tunapokaribia kurudi kwa Bwana Mara ya Pili, Mungu ameanza kuinua mitume **na manabii ambao watalipigia mbiu Neno la Mungu katika ufahamu na uwazi,** kuandaa kanisa kwa, na kuonya ulimwengu juu ya, tukio hili la ajabu.

Makundi ya Utume

Siku hizi **Mungu anawainua mitume**. Katika mitume, vikundi vya waaminio vinakusanyika ambavyo vimejitolea katika fundisho la mitume. Hivi sasa, **vikundi vya Utume** vinaanzishwa, ambavyo vinahusisha watu wote ambao wanatembea katika karama na huduma. Kwa hivyo kuna jambo ambalo liko linatendeka katika kutekeleza Ukristo wa Agano Jipya. Mitume sio wawakilishi wa kikundi Fulani cha kanisa, muondoko au dhehebu. Kwa hivyo hawafungwi na desturi, wako huru kutokana na mafundisho na matendo ya wanadamu. Kwa sababu hiyo, ni kwa njia ya vikundi vya utume, **Mungu yuko anainua mifano ya watenda kazi Wakikristo ambao ni wa Agano Jipya,** kutoa maongozi kwa kanisa zima, maongozi ya kurudia matendo ya Ukristo wa Biblia na kuandaa kanisa liwe tukufu, takatifu, bila mawaa, tayari kwa ajili ya kurudi Kwake.

Yanafanyika aje!

Katika muongozo huu, tutakuwa tukichunguza vile **yanavyo fanyika** katika jumuia ya Wakristo wa Agano Jipya: mambo kama ubatizo, Meza ya Bwana, fedha, kifuniko cha utume, kuwatawaza wazee, huduma ya nyumba kwa nyumba na kupanda makanisa mapya. Tunayo mafundisho kwa baadhi ya mambo hayo ya maisha ya Kikristo na mafunzo mengine katika miongozo mingine, lakini katika muongozo huu tutatafuta kuonyesha jinsi mafundisho ya kweli yanavyostahili kufanywa katika matendo. Ndiposa kichwa **“IMANI KATIKA MATENDO”**.

SURA YA KWANZA

UBATIZO
TUBUNI MKABATIZWE

TUBUNI MKABATIZWE

Je, ushawahi kutambua njia nyingi ambazo wainjilisti wengi wanatumia katika kuwaleta watu kwake Kristo ni tofauti sana na mfano wazi katika Maandiko Matakatifu? Je! Umeshawahi kusikia muinjilisti, baada ya kuhubiri Neno la Mungu, akiwaamurisha wasikilizaji ambao wameshawishika, ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipwa cha Roho Mtakatifu,"*** **Matendo 2:38**? Yesu mwenyewe alisema katika **Mk.16:15-16a** ***"Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka."*** Tena katika **Matt.28:18-20**, Yesu aliamuru mitume kwenda kuwafanya wanafunzi kwanza kuwabatiza kisha wawafundishe.

Tambua; tunafundisha baada ya ubatizo!

Makanisa mengi husisitiza kuwa wale ambao wameokoka [wachanga] waingie kwanza katika darasa la waongovu wapya kabla ya kubatizwa na wanafanya kuhudhuria hizo darasa kuwa kigezo kikuu cha kubatizwa. Wazi wazi hili ni kinyume na amri ya Yesu. Po pote katika kitabu cha **Matendo,** ubatizo ulifuata imani mara moja. **Mfano wa Biblia ni ubatizo kwanza halafu kufundisha ni pili.**

POKEA KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU

Tendo la wazi katika Maandiko Matakatifu ni kuwa wale wanaomuamini Bwana wabatizwe. Watu wanaokolewa kwa njia ya ***"kuamini na kubatizwa"*** (**Mk.16:16**). Siku ya Pentekoste, ni wale watu walioshawishiwa na Neno ndio Petro aliamuru kutubu na kubatizwa. Aliwaambia kuwa wakifanya hivyo, **watapokea kipawa cha Roho Mtakatifu**. Makanisa mengine hufuata mfano wa Maandiko Matakatifu kwa kubatiza tu lakini hawana matarajio kuwa walioamini watapokea ahadi ya Roho Mtakatifu.

Kupokea Roho Mtakatifu ni tendo

Katika kitabu cha Matendo, ubatizo ulifuata mara tu watu walipokuwa wameamini Bwana na kila wakati kulikuwa na matarajio kuwa yule aliye batizwa **atapokea Roho Mtakatifu katika njia inayo tambulika.** Kwa mfano, katika **Matendo 8:12**, waume kwa wake walioamini mahubiri ya Filipo walibatizwa. Hata hivyo, hawakupokea Roho Mtakatifu, hadi wakati ambapo Petro na Yohana waliposhuka kutoka Yerusalemu, ***"Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu"*** **a.17**. Simoni, Yule mchawi, aliona nguvu zikishuka kupitia kwa kuwekea mikono – **kitu hutendeka wakati mtu anapompokea Roho Mtakatifu wa Mungu**. Yesu alisema, ***"Mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu"*** **Matendo 1:8**.

Je! Ulipokea Roho Mtakatifu?

Kuna waaminio wenga sana kanisani leo ambao wamebatizwa lakini hawajapokea 'nguvu' za Roho Mtakatifu. Hili sio jambo la kithiologia wala fundisho la mpango lakini ni ukweli ambao wewe umeshuhudia ama haujaushuhudia. Ndipo Paulo aliwauliza wanafunzi huko Efeso, ***"Je! Mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?"*** **Matendo 19:2**. Wakamjibu, ***"la, hatakusikia kuwa kuna Roho Mtakatifu hatukusikia,"*** **a.2**. Kisha Paulo akawauliza juu ya ubatizo wao, kwa sababu **Paulo alitarajia kuwa wakati wa ubatizo waaminio wangepokea**

Roho Mtakatifu. Hawa wanafunzi ndio Paulo alibatiza tena baada ya kuwahubiria Yesu na wakamuamini.
Watu wengi wameupokea ubatizo wa kanisa ambao msingi wake ni kuwa mshirika wa hilo kanisa, lakini hawajawahi ***"Mwamini Bwana Yesu"*** **Matendo 16:31**, wapate kuokoka. Kwa hivyo ubatizo wao ulikosa nguvu – hawakupokea Roho Mtakatifu.

AMRI YA KUBATIZA

Amri ya kubatiza ilitolewa na Yesu baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, katika **Mt.28:19** ***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."***
Mk 16:16a ***"Aaminiye na kubatizwa ataokoka."***

Petro anatii amri
Kitabu cha **Matendo** kinatuonyesha utiifu wa Mitume katika kubatiza, mara tu watu walipoanza kuweka imani yao ndani yake Yesu Kristo. **Matendo 2:38** na **41** yanukuu ubatizo wa kwanza. Wale walioshawishiwa na mahubiri ya Petro waliuliza kuwa wafanye nini. Petro aliwaamuru watubu, wabatizwe na kusema mambo mawili muhimu kuhusu ubatizo:
1 ***"mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo"***
2 mbatizwe ***"kwa ondoleo la dhambi zenu"***.

PETRO ALISEMA MBATIZWE KATIKA JINA LA YESU KRISTO
Petro ni mmoja kati ya wale mitume kumi na mmoja aliyepokea amri hii Yesu alipoitoa katika **Matt.28:19**. Hapa kuna siri! Wengi katika kanisa leo na katika historia wamatumia maneno katika **Matt.28:19** katika ubatizo, ilhali **Petro aliwaambia wazi kuwa wabatizwe katika jina la Yesu Kristo**. Je, Petro alikuwa anaasi? **au je, Petro alikuwa na ufunuo kuhusu jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu lililokuwa limefunuliwa?** Hakika watu wote wanakubaliana kuwa jina la Mwana ni Yesu, (**Matt.1:21**).

Je, jina la Baba ni gani?
Baba sio jina, bali linaelezea nafasi au cheo cha mtu katika uhusiano. Katika **Kutoka.3:14** Mungu anamfunulia Musa jina lake kuwa ***"MIMI NIKO"*** na hilo jina wakati mwingi hutafsiriwa katika Biblia kama "**BWANA"**, wakati mwingine kama Yehova au ***Yahwe***.

Roho Mtakatifu Ana majina mengi ya kupendeza
Hakuna mahali po pote katika Maandiko Matakatifu ambapo Jina la Roho Mtakatifu limefunuliwa. Kristo maana yake ni ***'aliyetiwa Mafuta'***, likizumgumzia kupokea nguvu za Roho Mtakatifu Aliyemjilia Yesu kumwezesha kuitimiza huduma na Umasihi Wake (**Matendo 10:38**). Kusema ukweli, jina la Baba lililofunuliwa ni BWANA, na **Mungu amemfanya Yesu, Mwana, kuwa Bwana na Kristo** (**Matendo 2:36**). Cheo ***'Kristo'***, ambacho ni sawa na jina ***'Masihi'***, **linamaanisha Roho Mtakatifu aliye mjilia Yesu na kumtia Mafuta ili awa Kristo.**

Jina la Yesu ni Jina lipitalo majina yote!
Utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya kimwili unakaa ndini ya Kristo (**Kol.2:9**). Hili linamaanisha kuwa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanakamilishwa katika Jina Yesu Masihi. **Filip. 2:11** ***"na kila ulimi ukiri kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba."*** **Jina la Yesu ni jina alilopewa na Mungu ambalo linapita majina yote**, **a.9**. Ndiposa Petro alibatiza katika jina la Yesu Kristo. Mtume Paulo alikuwa na ufunuo uo huo, alipowabatiza waaminio wachanga katika **Matendo19:5** ***"katika Jina la Bwana Yesu"***.

KWA ONDOLEO LA DHAMBI

Petro alisema mkabatizwe kwa jina la Yesu Kristo, ***"kwa ondoleo la dhambi zenu"***, **Matendo 2:38**. Ondoleo linamaanisha *'kufutilia mbali'*. Petro alisema kuwa, kwa kubatizwa, dhambi zitaondolewa. Kufahamu haya zaidi ni katika **Rum. 6** ambapo Paulo anafafanua akisema, ***"tulibatizwa katika KristoYesu, katika mauti Yake,"* a.3**. ***"Tulizikwa pamoja naye katika njia ya mauti Yake"* a.4**, na tunafufuliwa katika mfano wa ufufuo Wake (**a.5**). **A.6** ***"Utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."*** Hivi ndivyo dhambi zetu huondolewa katika ubatizo. Katika ubatizo, tunapitia mauti, maziko na ufufuo katika Kristo Yesu na katika hali hiyo, utu wetu wa zamani ambao ni wa dhambi unasulubishwa. **A.7-8** ***"Kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi. Lakini tukiwa tumekufa na Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti hayamtawali tena."*** Huku kukufa na Kristo kunatendeka kwa njia ya Roho kulingana na Neno la Mungu katika ubatizo: **hakika dhambi zinaondolewa**.

UBATIZO WA KIKRISTO

Ubatizo wa kikristo ni tofauti na ubatizo mwingine wo wote. Ni tofauti na ubatizo wa Yohana ndiyo sababu Paulo katika **Matendo 19 aliwabatiza tena** walioiweka imani yao ndani yake Yesu, maana awali walikuwa wamepokea ubatizo wa Yohana. Je, ubatizo wa Yohana unatofautiana aje, na ubatizo wa Kikristo? Ubatizo wa Yohan ulikuwa katika maji **kama mfano tu**. Watu walibatizwa kama ishara ya mwili kwa kujiaandaa kubadilishwa ndani na kumpokea Masihi. Ubatizo wa Kikristo ni zaidi ya tendo la nje la kuwekwa ndani ya maji. Maandiko matakatifu yanafundisha wazi wazi kuwa **ubatizo ni tendo la kiroho pamoja na Kristo katika mauti Yake, kuzikwa na kufufuka.** Kiini cha ubatizo wa wa Kikristo ni Msalaba na ufufuo. **Kwa sababu Kristo alikufa na kufufuka tena ubatizo ni kufa na Kristo, na kuzikwa Naye [utu wa zamani umezikwa] na kufufuliwa katika upya wa uhai kwa njia ya ufufo Wake,** (**Rum.6:3-10**).

Ubatizo wa Kikristo ni wa watu walioamini peke yao, hivyo ni kusema, wale ambao wameoshwa dhambi zao na damu ya Yesu Kristo kwa njia ya imani ndani Yake, baada ya kuisikia injili. Ubatizo wa Kikristo ni ubatizo katika Kristo, katika Ufufo Wake na kwa hivyo mabatizo ya kanisa yanahitajika kuchunguzwa kulingana na **Matendo 19.**

Je, ulibatizwa katika Kristo?
Je, ulibatizwa katika kanisa fulani?
Je, ulibatizwa kulingana na msingi wa toba na imani?
Je, ulipokea kipawa cha Roho Mtakatifu ulipobatizwa?

MFANO WA UBATIZO WA YESU

Ubatizo wa Yesu niwa kipekee na ulikuwa Wake. Hakuwa anatimiza **ubatizo wa Yohana wa toba** [Yesu hakuwa na dhambi ya kutubu, na ubatizo wa Yohana ulikuwa wakuandaa watu ili wampokee Yeye]; bali alikuwa anajitolea ***"kuitimiza haki yote"* Matt.3:15**. **Hii haki ilikuwa haki kulingana na sheria ya Musa** ambapo **Yule aliyekuwa akiingia katika ukuhani alihitajika kutawadhwa** na kuhani [katika hali hii alihitajika awe Yule kuhani mkuu wa zamani, lakini Mungu alimchagua Yohana kumbatiza Mwana Wake]. Yule aliyekuwa anatawadhwa angetiwa mafuta na **Mungu mwenyewe alimtia mafuta Yesu Kristo awe Kuhani mkuu wa milele.**

Hata hivyo, kuna mfano wazi katika ubatizo wake Yesu ambao tunaweza kuufwata na tutarajie kukamilika ndani ya maisha yetu.

1. **Yesu alibatizwa kwa kumtii Mungu**;
   Tunatakikana kubatizwa kwa kuitii amri ya Yesu.
   Yesu alipopanda kutoka ndani ya maji,
2. **Alimpokea Roho Mtakatifu**;
   Tumeahidiwa Roho Mtakatifu tunapojitolea katika ubatizo, na baada ya kutubu na kumuamini Yesu Kristo. Roho Mtakatifu huwashukia watu kwa njia mbali mbali, kama: kunena katika lugha mpya, kuona maono, kupokea uguzo Wake wa nguvu
3. **Baba Mungu Wake alinena kwa sauti kuhusu Yesu, kuonyesha kuridhika, na kumtambulisha kuwa Mwana wa Mungu.**
   Tunaweza kutarajia unenaji wa kinabii katika ubatizo wetu, kukubaliana na kututhibitisha katika wokovo mpya. Kufikia hapo huwa tunahitaji kuwe na mashahidi, hasa wale ambao wamejaaliwa kutabiri, wawaombee wale ambao wamebatizwa wanapotoka ndani ya maji ya ubatizo.

Mfano kwa ufupi:

Ubatizwe kulingana na amri ya Yesu;
Tarajia kipawa cha Roho Mtakatifu – Atakupatia ishara wazi kuwa umempokea;
Tarajia Neno kutoka kwa Bwana juu ya maisha yako kukuhimiza na kukuthibitisha.

MAFUNZO ZAIDI JUU YA UBATIZO

1. Kuvikwa na Kristo

Gal.3:27-29 ***"Maana ninyi myote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.Hapana Myahudi wala Myunani, hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mtu mke, maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warihi sawa sawa na ahadi."*** Tumebatizwa katika Kristo; tumemvaa Kristo, hatutengwi Naye tena. Katika Kristo, mipaka yote ya kabila, hali za uchumi au jinsia zinaondolewa na tunakuwa mmoja katika Yeye. Kwa njia ya ubatizo tunakuwa warithi sawa sawa na ahadi aliyopewa Ibrahimu kwa sababu sasa tumo ndani ya Kristo ambaye ni Mbegu ya Ibrahimu, (**a.16**).

2. Ubatizo hauko sawa na tohara

Kol 2:11-12 ***"Katika Yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuuvua mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristo. Mkazikwa pamoja Naye katika ubatizo, na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu."*** Watu wengine hufundisha kimakosa kuwa ubatizo wa Kikristo kwa waaminio wa Agano Jipya ni kama tohara kwa watu wa Mungu katika Agano la Kale. Katika swala hili, huwa wanashindana kuwa kuiunga mkono na hata kuwabatiza watoto wachanga. Tohara inayozungumziwa katika Maandiko haya sio ya mwili bali ni ***"kwa kuuvua mwili wa nyama"***; hili hutendeka kwa njia ya ubatizo wa Kikristo na hutendeka tu kwa mtu ambaye ametubu dhambi zake na kuamini. Watoto wachanga wanatakikana wawekwe wakfu kwa Bwana kwa njia ya maombi. Kuwafanya watoto kuwa wakristo kwa kuwanyunyizia maji sio sawa na ubatizo. Wakati makanisa yanapofundisha kuwa watoto wanyunyiziwe maji ni ubatizo wa kweli, wanawanyima walioamini msingi wa kweli wa ubatizo wa Kikristo.

3. Ubatizo unatuokoa kwa njia ya ufufuo wa Yesu Kristo

1 Pet.3:20b-22 ***"Siku za Nuhu safina ilipokuwa ikitengenezwa, ambamo ndani yake wachache, yaani watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni ubatizo; unaowaokoa ninyi pia siku hizi [sio kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu] kwa kufufuka kwake Yesu Kristo."***

Mahubiri ya Petro yanatia nguvu mafundisho ya Paulo katika **Rum.6.** Paulo amefundisha kuwa tulifufuliwa Naye ilituenende ***'katika upya wa uzima*** (**a.4**), kuwa ***'tumeunganika na Kristo katika ufufuo'*** (**a.5**). Petro anatuonyesha kuwa kwa njia ya ubatizo tunaingia katika ufufuo wa Yesu Kristo katika njia ya kuokoka kama vile Nuhu na Nyumba yake walivyoingia katika safina na kuokoka ***"kwa maji"*** **1Pet.3:20**.

Tena Petro anaendelea kufundisha kuwa katika ubatizo katika Kristo tunafufuliwa pamoja Naye hadi ***"mkono wa kuume wa Mungu"***, juu kuliko malaika, mamlaka na uwezo. Haya yanathibitisha mafunzo ya Paulo katika **Efeso** kuwa ***"akatufufua pamoja Naye katika ulimwengu wa Roho, katika Kristo Yesu"*** **Efe.2:6**. Katika **Efe. 1:20-23**, Paulo anatuonyesha kuwa Kristo ameinuliwa ***"juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka na nguvu na usultani na kila jina litajwalo"***; kuwa Kristo ni Kichwa cha Kanisa na kwa hivyo Mwili wake ulifufuliwa pamoja Naye.

Ni katika ubatizo ndiyo tunafufuliwa na kuketishwa pamoja na Kristo katika ulimwengu wa Roho.

4. Ubatizo: njia ya Ushindi

Ubatizo unatupatia njia ya kumshinda shetani. Katika ubatizo **'utu wetu wa kale**, yaani, 'mtu wa maumbile ya zamani', Yule ambaye aliishi katika utumwa wa shetani, **amezikwa pamoja na Kristo na tunafufuliwa** 'kuwa **'mtu mpya' katika Kristo**. Kwa hivyo, mambo ambayo yalikuwa yakitusumbua katika 'mtu wa maumbile yazamani' hayana uwezo juu yetu tena. Shetani hupenda kutukumbusha udhaifu wetu na dhambi za yule 'mtu wa maumbile ya zamani', lakini hayo yote yalizikwa katika ubatizo. Kuna **kuwachanishwa na 'utu wa zamani' katika ubatizo ili tusitawaliwe tena na mambo yale ya zamani.** Wakati adui anapokuja na kutushitaki, tunaweza kusema *'La, shetani, mimi siye yule mtu tena, huyo mtu alikufa katika ubatizo, mimi sasa ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu'.*

Jinsi tu tunavyo uangalia msalaba wakati tumetenda dhambi baada ya kuokoka na kuitisha damu ya Yesu kutuosha dhambi zetu, tunaweza kurudi kwa ubatizo wetu wakati shetani anavyojaribu kutufanya kuwa na hatia au aibu juu ya mambo ambayo tumefanya, na tumkumbushe kuwa tumetenganishwa na 'mtu wa zamani' na sasa hana cho chote tena juu yetu cha kutushitaki.

MATENDO YA UBATIZO

NI NANI ANAYESTAHILI KUBATIZA?

Yesu aliwaamuru mitume kubatiza katika **Matt.28:19**; alikuwa akiwaambia wale wanafunzi kumi na mmoja. Katika **Marko 16:15-16** Yesu pia alikuwa akiwaambia wale kumi na mmoja lakini hakufanya ubatizo uwe kazi ya watu fulani. Katika **Matendo 8** Filipo ambaye alikuwa **ametawazwa kuwa msaidizi**, lakini anafanya uinjilisti huko Samaria, aliwabatiza wote walioamini. Hata hivyo katika hali hiyo, hakuwa na mamlaka ya kuwaombea kupokea Roho Mtakatifu, bali kulikuwa na ishara nyingi na maajabu ya uponyaji na ukombozi.

Katika **Matendo 9**, Anania, **mwanafunzi**, alimbatiza Sauli [baadaye Paulo] na kumwekea mikono ili Sauli apone na ajazwe na Roho Mtakatifu. Pia alimnenea Sauli Neno la unabii kutoka kwa Bwana.

Katika Maandiko Matakatifu, **mitume**, **msaidizi aliyewekwa wakfu**, **muinjilisti** na **mwanafunzi wote walibatiza**. Katika makanisa mengi, yule tu ambaye 'ametawazwa' anakubaliwa kubatiza na ubatizo unaofanywa nje ya mamlaka ya hilo kanisa unakuwa sio halali. Hii ni kwa sababu wakati mwingine ubatizo unasisitizwa kuwa watu wanabatizwa katika dhehebu fulani la kanisa fulani badala ya kubatizwa katika Kristo.

Hatusemi kuwa ye yote anaweza kubatiza. **Ubatizo wa kawaida ni kuwa yule ambaye ametawazwa, anayestahili kusaidiwa na wanafunzi hubatiza wale ambao wameamini wakiwa chini ya uangalizi.** Hata hivyo, kulingana na Maandiko Matakatifu ni ruksa kwa yule ambaye ni msaidizi aliyewekwa wakfu na mwanafunzi kubatiza wakati unapowadia.

NI NANI ANAYEBATIZWA?
Matendo 2:41 ***"Nao waliolipokea Neno Lake wakabatizwa."***
Matendo 8:12 ***"Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na Jina Lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume kwa wanawake."***
Matendo 8:37 ***"Tena Filipo akasema, 'ukiamini kwa moyo wako wote.'"***
Matendo 9:17-18 Sauli, **baada ya kukutana na Yesu** njiani, baada ya Anania kumhudumia, akasimama, akabatizwa.
Matendo 10:47 ***"Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?"*** **A 48a** ***"Akaamuru wabatizwe katika jina Lake Yesu Kristo."***
Matendo 16:14b-15a ***"Ambaye Bwana aliufungua moyo wake, ayatunze maneno yaliyonenwa na Paulo hata alipokwisha kubatizwa …."***
Matendo 16:31-33 ***"Wakamwambia, 'Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka … wakamwambia Neno la Bwana … kisha akabatizwa."***

Na je, watoto?
Swali la muhimu la kuulizwa ni: mtoto anatakiwa awe na umri gani ili aweze kuokoka? Ama kama hicho sio kipimo, itakuwaje wakati atakapojazwa Roho Mtakatifu na kuanza kunena katika lugha? Je, mtoto wa aina hiyo anaweza kunyimwa ubatizo? Mbona basi wengine wanawanyima wokovu watoto ambao wanataka kuokoka?

TUBATIZE LINI?
Siku iyo hiyo
Matendo 2:41 wale elfu tatu waliolipokea Neno walibatizwa **'siku hiyo'**.

Mara moja
Matendo 8:38 ***"Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akabatizwa."***
Matendo 10:44-48 Petro aliwaamuru mataifa waliokuwa katika nyumba ya Kornelio kubatizwa na mara moja alipoona wamejazwa Roho Mtakatifu.

Siku tatu baadaye
Matendo 9:9-18 Sauli kwa siku tatu alikuwa kipofu baada ya kukutana na Bwana Yesu na mara Anania alipokuja kwake na kumponya, alijazwa na Roho Mtakatifu na akabatizwa.

Saa ile ile ya siku
Matendo 16:33 askari wa gereza pamoja na jamii yake walibatizwa saa ile ile ya siku.

JINSI YA KUENDELEA
Kwa sababu desturi hufa haraka na wahudumu wengi hawaelewi ni jina gani lakutumiwa katika ubatizo [vikundi vingine vinavyobatiza katika Jina la Yesu wameshitakiwa kuwa wako kinyume na utatu mtakatifu] njia ambayo yaweza kutusaidia ili tufikie ufunuo mkamilifu wa Jina la Bwana ni kama ifwatavyo:

Kwenye ibada ya ubatizo, kwa ufupi fundisha ubatizo kutoka kwa Maandiko Matakatifu.

Ni vyma wakati mwingi kusoma juu ya ubatizo Wake Yesu na ujenge matarajio kwamba Yule ambaye atabatizwa atapokea Roho Mtakatifu. Hili tarajio la Roho Mtakatifu linathibitishwa zaidi na Petro katika **Matendo 2:38**.
Nukuu amri ya Bwana katika **Matt. 28:19**
Na mifano muhimu juu ya ubatizo katika Jina kwenye kitabu cha Matendo. [mifano ambayo ni wazi ni: **Matendo 2:38, Matendo 19:5**].

Ikiwa kuna wengi wa kubatizwa, muhudumu anafundisha na kufafanua na kunena juu ya ubatizo katika Kristo. Wakati unapowadia wa kuwaingiza katika maji, unahitaji kusema *"nakubatiza katika Jina la Yesu Kristo"*, baada ya kufafanua kuwa jina la Yesu lina mamlaka yote na utukufu wa Mungu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu wanafunuliwa.

Kila ubatizo ni wa kipekee. Hakuna ibada na ninataka niseme kuwa kama unafanya jambo hilo basi unafaya mambo ya dini maana hakuna 'ibada inayopangwa'! ubatizo mmoja ambao nimeufanya ulikuwa wa watu 69 huko Kenya, Afrika Mashariki. Mara nyingi nimembatiza mtu mmoja. Wakati waaminio ni wachache, unaweza kuchukuwa mda kwa kila mmoja.

Hata hivyo, mpangilio wa kawaida ni kama ifwatavyo:

1) **<u>Shiriki Maandiko machache</u> kuhusu ubatizo**
   Amri
   Ubatizo Wake Yesu
   Vile ilivyofanywa katika **Matendo ya Mitume**
   Fundisho ambalo ni muhimu katika **Rumi**
2) **<u>Batiza katika Jina la Yesu Kristo</u>, Bwana Yesu, au Bwana Yesu Kristo, ukimtukuza Mungu Baba, na Mwana na Roho Mtakatifu. Ubatizo ni katika Jina, katika Kristo Aliyetiwa Mafuta.**
3) **<u>Tarajia Roho Mtakatifu</u> kushuka na kudhihirika katika maisha ya kila mtu, *"mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*** Chukua wakati (hata kama watu ni wengi) kuombea kila mmoja wao anapotoka ndani ya maji kwa njia ya kuwekea mikono.
4) **<u>Kuwa na mashahidi</u> (wandugu wenye vipawa) kuwawekea mikono wanapotoka ndani ya maji.** Roho Mtakatifu anaweza kunena kiunabii juu ya mtu wakati huu.

NI WAKATI WA MABADILIKO

Neno la Mungu ni wazi: **batiza wakristo wachanga mara tu wanapompokea Yesu.** Ni tendo la kawaida kulingana na Biblia kubatiza **siku ile ile ambayo mtu amempokea Kristo**. Ubatizo ni hatua ya imani ya kwanza ya hakika wakati mtu anapomuamini Yesu. Maana mipango ya kanisa imetupokonya utiifu wa Maandiko Matakatifu na mifano yake, na hivyo ubatizo mwingi haufundishi au kuhudumiwa ipasavyo. Kwa sababu hiyo misingi ya imani haiwekwi inavyostahili na wakristo wengi huendela kuwa wanyonge na kumenyana kwa sababu hawana msingi imara. Wahudumu wengi ni wapumbavu, baada ya kusoma shuhuda katika biblia, wanaasi na kupuuza amri za Bwana Yesu na mifano ya mitume wa kwanza.

TUBUNI MKAMWAMINI YESU KRISTO
MKABATIZWE NA MPOKEE KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU

SURA YA PILI

KUUMEGA MKATE
IBADA ISIYOKUWA YA DINI

Siku hizi Mungu anarejesha 'Kumega Mkate' kwa watakatifu. Kumega Mkate kunajulikana kama Meza ya Bwana au Meza au chakula cha Bwana na katika makanisa ya juu kama Ekaristia. Katika makanisa mengi hata ya kipentekoste, Meza ya Bwana imefanywa kuwa sherehe ya dini yenye sheria nyingi ambazo zimewanyima watu **furaha, weupe wa moyo na upendo wa Meza**. Tendo hili limekuwa la labda mara moja kwa mwezi katika makanisa machache tu. Katika makanisa mengi mkate hauwezi kumegwa hadi muhudumu ambaye amewekwa wakfu wa dini hiyo yupo. Watoto wakati mwingi wanatengwa na kunyimwa Meza na wale ambao hawaja batizwa ambao wameamini pia hutengwa katika makanisa mengine.

Katika funzo hili tutaangalia Kuumega Mkate katika Maandiko Matakatifu, kufafanua ni nani anayestahili kupokea Meza na ni nani anaweza kuhudumu. Tutatoa mfano rahisi ambao tunafurahia kama watu wa Mungu, ambao tunajua unatokana na Maandiko Matakatifu.

MEZA NI SAWA NA USHIRIKA

1 Kor.10:16 ***"Kikombe kile cha Baraka tukibarikicho, je! Si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa Mwili wa Kristo?"***

Neno 'Meza' katika aya hiyo katika Kiyunani ni *'Koinonia'* ambalo ni sawa na neno la ushirika.

> SC # 2842: kushirikiana, umoja, uhusiano wa karibu, kuhusika, jumuia, Meza, ushirika, Chakula cha Bwana, mchango, undugu. *'Koinonia'* ni umoja ambao unaletwa na Roho Mtakatifu. Katika *'Koinonia'* mtu anashiriki vitu vyake vya kawaida katika ushirika wa karibu pamoja na jumuia ya wakristo. *'Koinonia'* unajenga uhusiano wa Mkristo na Bwana Yesu na kati ya mmoja na mwingine.

Paulo mtume anachangia katika swala hilo la ushirika katika **1 Kor.11** anaposisitiza juu ya kuupambanua Mwili wa Kristo wakati tunapokuja Mezani. Paulo anatuhimiza kungojeana na kujichunguza wenyewe kuhakikisha kuwa hakuna mgawanyiko katika mioyo yetu na wengine.

SISI SOTE NI MWILI MMOJA

1 Kor.10:17 ***"Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi ni mwili mmoja kwa sababu sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja."*** Kama vile wanaisraeli ***"wote wakala chakula kile kile cha roho, wote wakanywa kinywaji kile kile cha roho,"*** [ulikuwa ni Kristo] **a.3-4**, sisi sote ni washirika wa huo mkate mmoja. Sisi, japo wengi, ni mkate mmoja na mwili mmoja. **Hilo linaelezea juu ya kutambulika kama watu wa Mungu.** Kuna mwili mmoja tu na mkate mmoja kwa hivyo tunapomega mkate ni vema kukumbuka kuwa sisi ni sehemu ya watu wa Mungu, kwa sababu kuna Mwili mmoja tu, yaani, Kristo mmoja ambaye tunashiriki. **Hakuna kitu kama meza ya watu fulani au kikundi fulani cha waaminio.**

KUTENGWA KWA AJILI YA MUNGU

1 Kor.10:21 ***"Hamwezi kushirkiana katika meza ya Bwana na katika meza ya mashetani; hamwezi kushiriki meza ya Bwana na Meza ya mashetani."*** Tunatakikana kuwa watu ambao wametengwa kwa Bwana tunapoishiriki Meza Yake. **Meza ya Bwana ni ya**

waaminio peke yao. Kwa hivyo utafanya nini wakati kuna watu wasioamini katika mkutano ambapo mkate unamegwa pamoja? Kile kilicho cha muhimu ni **shiriki wazi wazi kuhusu kufa kwake Yesu msalabani, kwa nini na jinsi tunavyoweza kuokolewa kutoka kwa dhambi kwa kumuamini.** Halafu **wape nafasi ya kuokoka**: wapatie nafasi wale ambao hawajaamini nafasi ya kuja kwa imani na kuokoka. **Kisha wanaweza kushiriki katika Meza!** Hallelujah!! Lakini unasema, *'hawajabatizwa!'* ni wapi katika Maandiko Matakatifu ambapo Yesu au Paulo wanasema kuwa mtu lazima awe amabatizwa ili ashiki katika Meza ya Bwana? Yesu alimwambia yule mnyang'anyi msalabani kuwa utakuwa nami Paradiso – hapakuwa na nafasi ya kupokea ubatizo. Sisi hufundisha kikamilifu na kubatiza wanaoamini mara tu wanapoamini lakini hakuna andiko lo lote ambalo linamzuia ambaye ameamini kutokupokea Meza eti kwa sababu hajabatizwa.

HAKUNA FARAGA KATIKA MWILI WA KRISTO

1 Kor.11:17-19 ***"Lakini katika kuagiza haya, siwasifu, ya kwamba mnakusanyika, si kwa faida bali kwa hasara. Maana kwanza mkutanapo kanisani nasikia kuwa kuna faraga kwenu, nami nusu nasadiki; maana lazima kuwapo na uzushi kwenu, ili waliokubalika wawedhahiri kwenu."*** Hakuna faraga na migawanyiko katika Mwili wa Kristo. **Desturi za makanisa zimeleta migawanyiko katika Mwili na hivyo 'Meza' nyingi zimetengewa watu wa shirika au makanisa hayo.** Kunahitajika kuwepo kwa mabadiliko na urejesho katika Meza ya Bwana kulingana na Neno la Mungu.

a.20 ***"Basi mkutanikapo pamoja haiwezekani kula chakula cha Bwana."*** Chakula cha Bwana kinatakiwa kuwa mahali pa umoja, **hili ndilo lengo la kuja pamoja**.

a.21-22 ***"Maana kila mmoja hutangulia kutwaa chakula chake katika kule kula; hata huyu ana njaa, na huyu amelewa. Je! Hamna nyumbani za kulia na kunywea? Niwasifu? La! Siwasifu kwa ajili ya hayo."*** Chakula cha Bwana kilikuwa katika misingi ya kushiriki chakula pamoja, lakini hapa watu walikuwa wamegawanyika katika makundi ya faraga na hakuna aliye kuwa akingojea mwingine. Huu mgawanyiko katika vikundi waonekana kuwa uliletwa na uwezo wa kiuchumi – wengine walikuwa na chakula kikamilifu, wengine hawakuwa na cho chote nao matajiri hawakushiriki na maskini. Watu walikuwa wakishibisha njaa yao ya kimwili na kiu bila kuzingatia na kuheshimu Meza ya Bwana. **Kwa hivyo hakukuwa na chakula cha Bwana.**

UFUNUO WA MEZA

Mkate

1Kor.11:23*"Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa ninyi, yakuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate."* Paulo alipokea ufahamu wa ufunuo na tendo la Meza ya Bwana. Maelezo yake yanathibitisha na kuweka wazi yale ambayo Yesu ametupatia katika Injili.

Mwili Wangu

a.24 ***"Naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio Mwili Wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.'"*** Wakati tunapokula mkate, Maandiko Matakatifu yanatwambia mambo mawili: **mkate unawakilisha Mwili wa Yesu uliovunjwa msalabani** na **tunakula mkate kumkumbuka Yesu**,
Mateso Yake pamoja na kifo Chake kwa niaba yetu
Na pia **kuudhihirisha ukweli kuhusu Bwana aliyefufuka.**

Kikombe

a.25 ***"Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe akasema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu.'"*** Hili Andiko Takatifu latufundisha mambo matatu:

1. **kuna Agano Jipya**, yaani, makubaliano mapya kati yetu na Mungu;
2. **Makubaliano haya yametiwa muhuri na damu ya Yesu** ambayo inawakilishwa na kikombe;
3. **Tunatakiwa kumkumbuka Yesu**, kwa **kuimwaga damu Yake ili atuoshe dhambi zetu na kudhibitisha agano,** na **ukweli uliopo wa uwepo wake pamoja nasi.**

Tendo la unabii

1 Kor.11:26 ***"Mana kila mlapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo."*** Tendo la kushiriki Meza ya Bwana ni **jambo la ajabu la kinabii**.

Paulo anasema ***'kila mara'***; hii inamaanisha kuwa tunaweza kushiriki hili tendo la kinabii 'kila mara'. Wakati tunapokula na kunywa tunatangaza mambo mawili ya Kweli yaliyo ya msingi: **BWANA alitufi msalabani watu wote**; Alifanya jambo hili la ajabu kwa ajili yetu; na **BWANA ANARUDI hivi karibuni** kwa hiyo watu wa Mungu na ulimwengu mzima wakumbushwe bila kukoma. Kanisa kwa uaminifu limekumbuka kifo cha Yesu lakini halijahubiri kurudi **Kwake mara ya Pili** katika Meza.

YESU ANAJIFUNUA KATIKA KUMEGA MKATE

Katika maandiko ya **Luka** njiani kuelekea Emau, tunaona macho ya wanafunzi hao wawili yakifunguka wakati Yesu alipoumega mkate pamoja nao. **Lu.24:30-31** ***"Ikawa alipoketi nao chakulani, alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. <u>Yakafunguliwa macho yao, wakamtambua</u>; kisha akatoweka mbele yao," n***a **a.35** ***"Nao waliwapa habari ya mambo yale ya njiani, na vile <u>alitambulikana nao katika kuumega mkate</u>."***

Hata hivyo, tunaweza kutarajia ***'kumjua'*** Yesu katika kuumega mkate. Ni wakati wa uhusiano na Bwana aliyefufuka.

MEZA YA BWANA: CHAKULA CHA PASAKA KATIKA AGANO JIPYA

Ufunuo wa Meza ya Bwana uko katika misingi wa chakula cha Pasaka. Ulikuwa wakati wa chakula cha Pasaka Yesu alipokuwa na wanafunzi wake, Alipo ***"twaa mkate, akaubariki na akaumega, kisha akawapa wanafunzi wake na kusema, Twaeni mle, huu ni Mwili wangu,"*** kisha akatitwaa kikombe ***"akawapa, akisema 'Nyweni nyote katika hiki. Kwa maana hii ni damu Yangu ya agano jipya imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi.'"*** **Matt.26:26-28**. **Marko**, **Luka** and **Yohana** wote wanathibitisha kuwa chakula cha kwanza cha meza kilikuwa kulingana na desturi ya hakula cha Pasaka. Hili linathibitisha mambo mawili:

Meza inasherehekewa katika msingi wa chakula cha ushirika
na kuwa **Yesu anatimiza Pasaka katika Meza.**

Pasaka ya kwanza ilikuwa wakati ambapo Mungu aliwakomboa Watu Wake, Waisraeli, kutoka kwa mharibifu kule Misri. Waisraeli **walilindwa nyumbani mwao na damu ya Mwana kondoo.** (**Kutoka.12**). **waliila nyama ya Mwana kondoo katika kujitayarisha kwa safari ya kuondoka Misri.**

Walikombolewa kwa mwili na damu ya Mwana Kondoo.

Tangu wakati huo, Waisraeli waliikumbuka Pasaka kulingana na Amri ya Bwana. Yesu alitamani sana kuila Pasaka pamoja na wanafunzi Wake (**Lu.22:15-16**). **Alijua umuhimu wa sikukuu hii na ingetimia tu kwa kifo Chake msalabani.** Mkate na divai vilikuwa ni viungo muhimu vya chakula cha Pasaka, vikiwakilisha siri ambayo Sikukuu hii ilielekezea. **Yesu aliutwaa mkate na divai na kufunua maelezo ya kutimia kwake katika kifo chake msalabani.**

Msaliti alikuwepo mezani pa chakula
Katika **Mk. 14:22-26**, Marko anaelezea pia kuhusu Meza ya Bwana, na Luka pia anatoa habari yake katika **Lu.22:14-23** wakifunua kuwa Yuda, msaliti, alikuwa mezani pa chakula cha Pasaka. Yohana anatoa habari kwa mapana kuhusu chakula cha Pasaka. Katika **Yoh.13:18-30** Yesu anamtambua atakaye msaliti, ***"Ndiye mtu Yule nitakayemtowelea tonge,"* a.26**. Je! Ukweli huu unaweza kutuonya kuhusu kuweka sheria kuhusu ni nani anayestahili na asiyestahili kuila Meza?

Mengi hutendeka Mezani!
Mafundisho ya Yesu katika **Yoh. 13-17** yalitolewa kwa misingi ya chakula cha Pasaka. Yesu alichukua fursa ya chakula hiki cha mwisho, **kutoa maagizo mengi na mafundisho kwa wanafunzi Wake.** Ni katika sura hizi katika Yohana ambapo Yesu **anazungumzia wazi wazi kuhusu kuja kwa Roho Mtakatifu na utu wake na huduma Yake.** Yesu **aliwatawadha miguu wanafunzi Wake**, (**Yoh.13:1-17):** katika msingi wa Meza ya Bwana hili linatwambia **Kungojeana, kuupambanua Mwili wa Bwana na kumpokea kila momoja** ambaye yuko mezani, kama kiungo muhimu cha Mwili.

INAMAANISHA NINI 'KUJIHOJI' MWENYEWE?

Mafunzo katika **1 Kor.11:27-34**
a.27 ***"Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana."*** Paulo anatwambia katika mistari iliyotangulia kuwa kuna tendo la kinabii katika kula na kunywa. Kwa hivyo hatustahili kuchukulia swala la Meza kwa wepesi au tutahukumiwa.

a.28 ***"Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate na kukinyea kikombe."*** Wakati tunapokuja Mezani pa Bwana ***"tujichunguze"*** wenyewe kabla ya kuila Meza. Hivyo ni kusema, angalia moyoni mwako, laikini twachunguza nini?

a.29 ***"Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili."*** Tunatakiwa **'kujichunguza'** wenyewe kuhusiana na ***"kuupambanu Mwili wake Bwana."*** Hili linamaanisha Mwili wote wa Kristo na si mwili wake wa asili ambao ulivunjwa msalabani. Chakula chaMeza ni chakula cha ushirika. Ni tendo ambalo linajumuisha watu wote na kila sherehe ya Meza ni tendo la kinabii kwa Mwili wote. Kwa hivyo tunapokuja Mezani, tunastahili kujichunguza miyoni na kuondoa kila faraga, kutokusamehe, mawazo mabaya kuwahusu wengine katika Mwili wa Kristo wawe wapo au la.

Ikiwa tutahusika katika Meza ambayo ni ya kipekee ambayo ni ya faraga, tutakuwa hatuupambanui Mwili. Maana kanisa katikka vizazi limesherehekea na kuhalalisha na kugawanya chakula cha Meza, kanisa kwa jumla ni nyonge na haliwezi na hata limekufa.

a.30-31 ***"Kwa sababu hiyo, wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu, na watu kadha wa kadha wamelala. Maana kama tungejipambanua nafsi zetu tusingehukumiwa."*** Kama "***hatuupambanui mwili"*** ipasavyo, tutakula na kunywa hukumu juu yetu sisi wenyewe.

a.32 ***"Ila tuhukumiwapo, twarudiwa na Bwana, isije ikatupasa adhabu moja na dunia."*** Kuhukumiwa ni kurudiwa na Bwana, na kusudi lake ni kuleta mabadiliko na haki katika maisha yetu.

a.33 ***"Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo mpate kula, mngojeaneni."*** Ushauri hapa ni "***kungojeana"***. Huu ni wakati wa umoja, msingi wake ni msamaha, kushirikiana na upendo wa mwili.

KUMEGA MKATE KATIKA MATENDO YA MITUME

Katika **matendo 2:42** tunapata kuwa ***"kuumega mkate"*** ulikuwa mojawapo wa ***"matendo ya kwanza"*** ambayo kanisa la kwanza ***"lilidumu"*** ndani yake. Hili lilikuwa ni tendo la kila siku katika nyumba, **a.46** ***"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe."*** **Wakristo wa kwanza walikutana kila siku nyumbani** na **kumega mkate kila siku nyumbani**. Hata kama kuna ushahidi kuwa makanisa yaliitambua siku ya kwanza ya juma [Jumapili] kama wakati maalum wa kukusanyika na kumega mkate, bila shaka kanisa la kwanza lilimega mkate kila siku nyumbani. La muhimu kwa urejesho kwa Ukristo wa mitume ni urejesho wa kuumega mkate nyumbani mwa kila mwamini wakati wakutanikapo.

UKRISTO WA KIMITUME KATIKA MATENDO

Msingi wa **mistari 42-47** watuonyesha **ukristo wa kimitume katika matendo**. ***'Walikuwa pamoja'***; wakazishudia ***'ishara na ajabu nyingi'*** miongoni mwao; ***'walishirikiana vitu walivyokuwa navyo'*** mmoja kwa mwingine; ***'wakimsifu Mungu'*** na ***'wakawapendeza watu wote'***. ***"Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa,"*** **a47**.

Kumega mkate kila siku nyumbani kulikuwa sehemu muhimu katika uhai wa kanisa

Kumega mkate ni mojawapo wa matendo ya kwanza ambayo kanisa a kwanza lilifanya. Matendo ya kwanza yamenukuliwa katika **Matendo 2:42**:

- **Fundisho la mitume** – mitume walihudumu nyumba kwa nyumba, kama vile Paulo alivyofanya baadaye kule Efeso, (**Matendo 20:20**);
- **ushirika** – huu ulikuwa ushirika wa ndani sana kwamba hakuna mtu aliyekosa cho chote;
- **kuumega mkate** – hii bila shaka ni Meza ya Bwana;
- na **kusali** – walishiriki maombi katika nyumba kila siku.

Katika **Ufu.2:1-7**, Yesu anakemea kanisa la Efeso kwa kuwa ***"limepoteza upendo wa kwanza"***. Anawaamuru ***"kutubu na kufanya matendo ya kwanza"***. **Njia ya kurudia uhusiano na Yesu, kumpenda kwa kweli, ni kwa kufanya matendo ya kwanza.** Huku ni kusema tukutane kila siku, ***"kudumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika na katika kuumega mkate na katika kusali."***

Siku ya kwanza ya juma

Matendo 20:7 ***"Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokutana ili kumega mkate …"*** wanafunzi "***walikutana" "kumega mkate"***. Inaonekana kuwa hii ilikuwa tabia ya kawaida ya wanafunzi. Kifungu hiki kinataja kuwa walikutana ***"siku ya kwanza ya juma"***. ***"siku ya kwanza ya juma"*** pia imetajwa katika **1 Kor.16:2** kua siku ya matoleo, ***"Siku ya kwanza ya***

juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadri ya kufanikiwa kwake ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja." Labda jumapili ilijitokeza kama siku maalum ya kukusanyika kumkumbuka Yesu. Mikusanyiko ya aina hii ilihuzisha nafasi ya ya kuchanga na wakati wa ujumbe wa Neno la Mungu.

Maisha ya ufufo hupatikana katika Meza

Hapa katika **Matendo 20** Paulo anawaonya na kuwaaga wanafunzi kule Troa. Katika mahubiri yake kijana mmoja alifufuliwa baada ya kuanguka kutoka dirishani; Maandiko Matakatifu yanaendelea kusema, ***"Akapanda* [Paulo] *juu tena, akamega mkate, akala, akazidi kuongea nao hata alfajiri, ndipo akaenda zake"* a.11**.

Kumega mkate katika hari na shari

Matendo 27:35-36 Merikebu ambayo Paulo alikuwa ameabiri ilikuwa imeadhirika kwa majuma mawili na mawimbi mazito baharini na sasa inavunjika. Lakini Mungu alikuwa amenena na Paulo usiku kupitia kwa malaika, na kwa hivyo alijua kuwa kuna ukombozi kwa ajili ya wote waliokuwa kwenye merikebu. Baada ya kuushiriki ushuhuda na wale mabaharia wengine ***"Akatwaa mkate akashukuru Mungu mbele yao wote, akaumega akaanza kula, ndipo wakachangamka wote, wakala chakula wenyewe"***. Kuumega mkate lilikuwa tendo la kinabii, akiwashuhudia wote [wengi wao walikuwa hawajaokoka] juu ya uaminifu wa Mungu.

Je! Umeshawahi kuongozwa kuumega mkate katika njia ya kuw ashuhudia waliopotea juu ya nguvu za wokovu wa Mungu?

KUTAJWA KWA MKATE MARA YA KWANZA KATIKA MAANDIKO MATAKATIFU

Kutajwa kwa mkate mara ya kwanza na divai kuhudumiwa ni katika **Mwa.14:18-20**. Melkizedeki alipokutana na Ibrahimu na akamuhudumia mkate na divai kama kuhani wa Mungu Aliye Juu. Katika msingi huu wa Mkate na Divai kuna:

Ufunuo wa Mfalme na Kuhani;
Kuna Baraka katika jina la Mungu Aliye Juu sana kwa mtu wa imani;
Hapa kuna fungu la kumi la kwanza katika Biblia.

Kutoka kwa huu msingi tunapata **mfano wa kumtolea Mfalme na Kuhani baada ya kupokea mkate na divai**. Ni ajabu sana wakati tunapoleta zaka zetu na sadaka kwake Yesu baada ya kumkumbuka katika Meza.

MEZA YA MKATE WA WONYESHO

Meza ndani ya Hema ya Musa ilijulikana kama Wonyesho, ambayo iliandikwa na mikate pamoja na divai (**Kut.37:16**). Hii inatuelekeza kwa Meza ya Bwana katika Agano Jipya. Ni muhimu kujua kuwa mkate na divai vilishikilia sehemu kubwa katika nyumba ya Mungu, wala sio katika ua wa nje, lakini katika Mahali Patakatifu. Hata hivyo, mkate wa wonyesho unajulikana kama ***'mkate wa uso'***; **uso wa Bwana ulifunuliwa Mezani.**

Hata Bwana wetu Yesu Kristo anajulikana kwa karibu katika Meza ya Bwana.

NI NANI ANASTAHILI KUPOKEA MEZA?

Kila anayeamini anaweza kupokea Meza

Katika **Matendo 2**, Wakristo wachanga ***"walidumu … katika kuumega mkate"* a.42**. Hakika walioamini walibatizwa siku hiyo ambayo walikuwa wamempokea Yesu. Kwa sababu kanisa la kihistoria na la kisasa yameshindwa kuwabatiza wanaookoka mara tu wanapookoka, wamekuwa na shida ya 'waaminio ambao hawajabatizwa' na wamewazuia hawa kuipokea

Meza ya Bwana. Shida ni ya huduma ya kanisa ambayo imeshindwa kubatiza kulingana na Maandiko Matakatifu. Kufunika kosa ambalo wamefanya kinyume na Maandiko, wamejitungia sheria kuihusu Meza. Ikiwa watabatiza kulingana na Maandiko Matakatifu hakungekuwa na haja ya sheria hizo na sheria hizo ni kinyume na Maandiko hata hivyo.

Na je, watoto?
Katika Injili, watoto waliletwa kwa Bwana ili awabariki, lakini wanafunzi wakajaribu kuwazuia. Yesu akawakemea na kuwaambia, ***"acheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa kuwa watu kama hao ufalme wa Mungu ni wao."*** **Lu.18.15-16**. **Je! Unafikiri Yesu anafurahi wakati tunapowazuia watoto wanapokuja Mezani pa Bwana?** Tofauti ni gani? Je! Sisi hatufanyi kama wanafunzi? Je! Tunastahili kukemewa na Bwana? **Mtoto anatakiwa kuokoka kwa umri gani?** Yesu aliendelea kusema, ***"Amin, amin, nawaambia, mtu ye yote asiyeupokea ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hauingii kamwe,"*** **Lu.18:17**. Ikiwa unaamini mtoto anaweza kuokoka akiwa na umri mdogo, na wanaweza, mbona basi tunawawekea mipaka katika Meza? Nimeshuhudia watoto wa umri mdogo wa miaka kama minne na mitano wakiwa na maono makubwa ya Roho Mtakatifu, hata kunena kwa lugha, kuwaona malaika, wakiongea na Yesu, na kuwa na maono ya Mbinguni!

Hakika Yesu anataka tuwahuzishe watoto na tuwe kama watoto wadogo sisi wenyewe kumpokea Yesu na Ufalme Wake.

NI NANI ANAWEZA KUHUDUMU MEZA?

Huduma ya madhabahu katika Agano la Kale ilikuwa imetengewa makuhani ambao walikuwa wamewekwa wakfu na kutiwa mafuta kwa ajili ya hiyo kazi. **Katika Agano Jipya waaminio wote** [wale ambao wametubu na kumuamini Yesu, wamebatizwa katika Yesu Kristo, na wamepokea kipawa cha Roho Mtakatifu] **ni makuhani**. **Ufu.1:5-6** yatwambai wazi kuwa **Yesu Kristo ametufanya kuwa makuhani**. Petro pia anatuita makuhani katika **1 Pet.2:9**. Chini ya Agano la Kale **makuhani ndio wale waliokuwa wakihudumu pale kwenye madhabahu** na katika Agano Jipya **ni makuhani wanaohudumu Mezani pa Bwana.** Chini ya Agano la Kale ilikuwa ni **makuhani wale waliokuwa wakihudu kwenye madhabahu ndio waliokuwa na haki ya kula sadaka**. Mtu mwingine ye yote hakuruhusiwa. Katika Agano Jipya **ni makuhani [waaminio wa kweli] wanaohudumu Meza ya Bwana, wana haki ya kupokea au kuila**.

Wale wanaoila ni wale wanaohudumu! Halleluyah!

MATENDO YETU

Tangu Bwana atuite kutoka katika dhehebu la kanisa mwanzo wa mwaka wa 1998, Alitupatia **uhuru wa kumega mkate katika ushirika wa waaminio, kila siku, nyumba kwa nyumba hata wakati tunapokuwa tunasafiri, ndani ya gari au kwenye ndege.** Tumeshuhudia **urejesho wa kanuni hii ya ajabu ambayo Bwana alianzisha kwa ajili ya kanisa Lake.** Yesu alipeana mkate bure kwa wale ambao watakuja kwa njia ya imani Kwake. Kumbuka alisema kuwa ***'damu Yake ilimwagika kwa ajili ya wengi'***. Sisi ni baadhi ya wengi ambao wamekuja Kwake kwa njia ya Imani.
Kumega mkate ni muhimu tena ni msingi kwa ajili ya uhai wa kanisa. Kwa kweli **wakati ambapo waaminio wanapoumega mkate pamoja** ndipo **kanisa linathibitika** kwa sababu **Yesu anawakilishwa katika kuumega mkate kwa njia kuu ya kipekee.** Haya yanatendeka kulingana na ahadi Yake katika **Matt.18:20** ***"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao."***

Kuumega mkate nyumba kwa nyumba

Tunapokuwa tukihudumu nyumba kwa nyumba, tumekuwa tukishiriki mkate kama sehemu ya mikutano yetu pamoja. Hili huwa ni jambo la ajabu kwa wale ambao wamekuwa katika misingi ya sheria za madhehebu ambayo yamezuia kumega mkate mahali ambapo si kanisani au bila aliyewekwa wakfu. **Uhuru wa kumega mkate katika ushirika wa kawaida wa wapendwa ni kwa neema.** Tuna wahimiza jamii na wakristo kwa jumla kuumega mkate katika nyumba zao kila mara, kila siku wakichagua na sio tu wakati wanapotembelewa na wapendwa katika ushirika bali liwe jambo la maisha ya kila siku kwa maisha ya Mkristo.

SURA YA YATU

ZAKA – UFUNUO WA IMANI

UTANGULIZI

Sijakosa kukutana na watu, hata wahudumu, ambao wanakiri kuwa kutoa zaka sio katika Agano jipya na kwa hivyo isitendwe. Hawa ndio huendela na kuwaambia watu kuwa wanafuata maufundisho ya Paulo juu ya kutoa, na hiyo ndio njia ya Baraka. Wazo lao ni kuwa kutoa zaka ni jambo la kisheria na kutoa sadaka ni kuwa huru. Ninatambua kuwa wapendwa kama hawa wamefungwa na hawana ushuhuda wa upaji wa Mungu. Katika funzo hili, tutatafuta kunena neema na imani kutoka kwa Mungu kwako, tukikuwachilia katika Neno la Mungu na uanze kutoa Zaka tena na sadaka ili upokee ujira wako ambao Ametuahidia.

KUTOA ZAKA KATIKA AGANO LA KALE

ZAKA YA KWANZA KATIKA MAANDIKO

Mwa.14:18-20 inatufundisha kuhusu Abramu akikutana na Milkizedeki. Milkizedeki alikuwa ***'mfalme wa Salemu'*** na ***'Kuhani wa Mungu aliye juu sana'***. ***'Akaleta mkate na divai'*** na kumpa Abramu. Akatangaza Baraka juu ya Abramu akisema, ***"Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi. Ahimidiwe mungu Aliye juu sana, aliyewatia adui zako mikononi mwako."*** Abramu alimuitikia Milkizedeki kwa kumpa fungu la kumi la vitu vyote. Na hii ndio zaka au fungu la kumi la kwanza katika Maandiko Matkatifu.

Melchizedeki ambaye ni Mfalme na Kuhani, Alimbariki Abramu ambaye ndiye *'baba wa imani'*, **Ebr.7:1-3** ***"Kwa maana <u>Milkizedeki huyo</u>, mfalme wa Salemu, Kuhani wa Mungu Aliye juu sana, Aliyekutana na Ibrahimu alipokuwa akirudi katika kuwapiga hao wafalme, <u>akambariki</u>; ambaye <u>Ibrahimu alimgawia sehemu ya kumi ya vitu vyote</u> ,tafsiri ya jina lake kwanza ni mfalme wa haki, tena mfalme wa Salemu, maana yake mfalme wa amani, hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu; huyo adumu kuhani milele.*** Ibrahimu alipokea ufunuo wakutoa fungu la kumi miaka mingi kabla torati ya Musa, na zaka au fungu la kumi la Ibrahimu ndilo linalozungumziwa katika Agano Jipya.

YAKOBO, MTOA ZAKA

Katika **Mwa. 28:10-22** Yakobo anakuta na BWANA. BWANA anamnenea katika njozi na kumbariki, akimuahidi baraka aliyopewa babu yake, Ibrahimu na baba yake Isaka. Yakobo alikukuwa na ufunuo kuhusu Mungu alivyo, **a.16** ***"Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, kweli BWANA yupo mahali hapa, wala mimi sikujua."*** **a.17** ***"Naye akaogopa sana, akasema, mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka , hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndilo lango la mbinguni."*** Hii ilikuwa njia ya Yakobo ya wokovu. Yakobo kuitikia wokovu wa Bwana ni kumjengea madhabahu. Alipaita mahali pale ***'Betheli'*** maana yake *'nyumba ya Mungu'*, na kuweka nadhiri kwa BWANA. ***"Mungu akiwa pamoja nami, akinilinda katika njia niendayo, na kunipa chakula nile, na nguo nivae; nami nikirudi kwa amani nyumbani kwa baba yangu, ndipo BWANA atakuwa Mungu wangu, na jiwe hili nililolisimamisha kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu; na <u>katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi</u>."*** **a.20-22**.

Kujitolea kwa Yakobo kwake BWANA kulihusisha kutoa fungu la kumi katika kila kitu alichokuwa nacho. Yakobo aliupata huu ufunuo wa fungu la kumi miaka mingi kabla ya Musa kupeana torati. Kwa mtoto wa Mungu, fungu la kumi sio sheria bali ni imani.

Fungu la kumi ni kuitikia imani kutokana na ufunuo wake Yesu Kristo

Ibrahimu pamoja na Yakobo walitoa fungu la kumi kwa Bwana kwa kuitikia ufunuo wao binafsi kutoka kwa Bwana. Kwa Yakobo ulikuwa sawa na wokovu wake. Kwa hivyo kuna mfano ulio wazi kwa ajili ya kila Mkristo mchanga kuufwata: mara tu mtu anapoupata ufunuo wa Yesu Kristo, ni kulingana na Maandiko Matakatifu yeye kutoa fungu la kumi kwa Bwana katika vyote anavyo pokea kutoka wakati huo kuendelea. Watu wengine husema, 'ninangojea ufunuo ili nianze kutoa fungu la kumi!' ufunuo tayari ni wazi katika Neno la Mungu na **unahitaji tu kutii kutokana na imani hiyo na utaongozwa kutoa fungu la kumi**.

KUTOA FUNGU LA KUMI CHINI YA SHERIA

Fungu la kumi chini ya sheria imenukuliwa katika **Walawi.27:30** ***"tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, ama kama ni matunda ya nchi, ni ya BWANA, ni takatifu kwa BWANA."*** Hii ilikuwa amri ya BWANA aliyompa Musa katika mlima wa Sinai, **a.34**.

Kimsingi **zaka ni takatifu kwa BWANA**, yaani, inawekwa kando kwa sabau ya makusudi ya Mungu. Ilitumiwa kwa Walawi ambao hawakuwa na urithi. **Hes. 18:21 "*Na wana wa Lawi, nimewapa zaka yote katika Israeli kuwa urithi wao, badala ya huo utumishi wautumikao, maana ni huo utumishi wa hema ya kukutania*."** **Walawi** kama kabila walikuwa **wametengwa kuwa wahudumu, makuhani, na waalimu wa torati** kwa Israeli yote na kwa hivyo waliishi kwa hiyo zaka iliyotolewa na makabila yale mengine.

Sehemu ya ile zaka ilitumiwa kwa ajili ya kuwasaidia wajane, mayatima na wageni. **Kumbu.14:28-29** ***"Kila mwaka wa tatu, mwisho wake, toa fungu la kumi lote la maongeo yako ya mwaka huo, uliweke ndani ya malango yako; na mlawi kwa kuwa hana fungu wala urithi pamoja nawe, na mgeni, na yatima, na mjane aliyefiliwa na mumewe, walio ndani ya malango yako, na waje wale na kushiba; ila kwamba BWANA, Mungu wako, akubarikie katika kazi yote ya mkono wako uifanyayo."***

CHANGAMOTO, MAREKEBISHO NA AHADI

Katika **Malaki 3:5-7** Mungu kupitia kwa nabii wake ananena na watu wake, akiwaambia kuwa wamemwacha na kwa sababu hiyo, mambo mabaya yamekuwa yakitendekea. Hukumu imekuwaikija juu yao. Mungu anawapa changamoto watu Wake wamurudie Yeye. Nao watu wanauliza, ***"turudi kwa namna gani?"***

Kumuibia Mungu

Katika **aya ya 8** Mungu anawapa changamoto nyingine kuwa, ***"Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mmeniibia mimi!"*** Walikuwa wakimuibia Mungu kwa njia gani? Walikuwa wakimuibia kwa njia ya kukosa kuleta zaka zao na sadaka[dhabihu] Kwake. Matokeo ya hayo ni kuwa, **a.9** ***"Ninyi mmelaaniwa na laana, maana mmeniibia Mimi …"***. Kwa kukosa kulipa zaka zetu tunamuibia Mungu nafasi ya kutubariki na Yeye kujithihirisha kwa ulimwengu kupita kwetu sisi.

Leteni zaka kamili

Aya ya 10 ina ahadi, ***"leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni Baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha au la.."***

Zaka ni fungu la kumi
Mungu anasema kuwa watu walete zaka, fungu la kumi ya yote waliyopokea, ghalani Mwake.

Ghala ni nini?
Katika misingi ya hili funzo ilikuwa ghala la nafaka. Hii ilikuwa jumuia ya wakulima na zaka ilikuwa wakati wote katika nafaka. Hii ilikuwa zaka ya asili na kwamba kungekuwa na chakula halisi katika nyumba ya Mungu. Hata leo katika nchi zinazoendelea wakati zaka inapotolewa, watu huleta nafaka, mayai au matunda kama zaka kwa Bwana.

Kanuni ni kwamba zaka iliwezesha chakula kupatikana ghalani, kuwalisha watu wa Mungu. Leo hii hatuji nyumbani mwa Bwana kwa chakula cha tumbo lakini kwa chakula cha kiroho. **Ghala letu ni ushirika tunaohudhuria, ama huduma tunayopokea chakula au lishe kutoka kwayo**. **Wahudumu ambao Mungu ameinua kutulisha kiroho wataishi katika zaka hizo**, ili wajitolee wenyewe katika maombi na kusoma Neno, kuhakikisha kuwa kutakuwepo na mtiririko wa chakula cha kiroho kwa ajili ya watu. (**Matendo 6:4**).

Amini kile Mungu anasema
Mungu anasema jambo la ajabu katika **a.10**. Anasema kuwa ***'tumjaribu'*** katika hilo. Huu ni wakati wa pekee katika Maandiko ambapo Bwana anasema tumjaribu. Anataka tumtolee zaka zetu na tumuone akitimiza ahadi, ambayo ni ***"kufungua madirisha ya mbinguni"*** na ***"kuwamwagia baraka hata kusiwe na nafasi ya kutosha."***

Mungu anamkemea shetani
Mungu pia anaahidi kumkemea alaye kwa ajili yetu. "***Nami kwa ajili yenu nitamkemea yule alaye, wala hataharibu mazao ya arthi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema BWANA wa majeshi,"*** **a.11**.
Yule **'alaye' ni adui yetu shetani**, (**1 Pet.5:8**).

Mungu anaahidi maongezeko
Wakati tunapomtolea Bwana zaka tunaweza tarajia baraka. Ameahidi maongezeko. "***Mazao ya arthi yenu"*** hayataharibika. ***"Wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba."*** Hizi Baraka zimo katika mambo ya kilimo ambayo bado inafanya kazi katika wakulima siku hizi, na baraka pia ni halali kwa mtu yeyote anayetoa zaka: Baraka juu ya biashara, kazi, jamii.

Toa kwa matarajio
Mungu anataka tuwe na imani ya matarajio kila wakati tunapotoa. Zamani, watu wengine wametoa kwa sababu ni kama sheria au wajibu. Fungu la kumi limefunzwa zaidi kama kanuni au sheria kuliko imani. Tunapotoa tunastahili kutarajia [jaribu Mungu] Mungu kutubariki. Matokeo yatakuwa ni kwamba tutajulikana kama watu waliobarikiwa, ***"'Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema BWANA wa majeshi."*** **a.12**.

Neno la Mungu halibadiliki! Mtu akitoa zaka kwa imani, huyo atapata dhawabu!

FUNGU LA KUMI KATIKA AGANO JIPYA

Yesu anatarajia fungu la kumi
Yesu anatarjia watu kutoa fungu la kumi. Katika **Matt.23:23,** Yesu alikuwa akinena na Mafarisayo na waandishi**,** "***mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha***

mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache." Yesu anasema **'*hayo imewapasa kuyafanya.*'** Kuna matarajio yaliyo wazi kutoka Kwa Bwana Yesu kuwa zaka ifanywe,' ***Lu.11:42.***

Baba wa imani alilipa zaka

Ibrahimu alilipa zaka kwa Melkizedeki kwa imani, (**Ebr.7:1-3**). Wakati tunapokuja kwa imani katika Kristo tunamtolea zaka Yesu. **Ebr.7:5-10** yaendelea kutuonyesha kuwa wana wa Lawi, ukuhani, walipokea zaka kulingana na sheria, bali wao pia walitoa zaka katika Ibrahimu. ***"Hata Lawi, apokeaye sehemu ya kumi alitoa sehemu ya kumi, kwa maana alikuwa katika viuno vya baba yake, hapo Melkizedeki alipokutana naye".*** **a.9-10**.

Melkizedeki kama ufunuo wa Yesu, alipokea sehemu ya kumi

Melkizedeki alikuwa kama mtu wa milele, hakuwa ***"na baba, wala mama, wala wazazi, hana mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa uhai wake, bali amefananishwa na Mwana wa Mungu,"*** **Ebr.7:3**. Yesu ni ***"kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki."*** **Ebr.7:17**. Kama Mfalme na Kuhani Yesu anapokea zaka zetu tunapomwendea kwa imani.

Ibrahimu akimtolea zaka Melkizedeki ilikuwa kwa imani; **ilikuwa kabla ya sheria**.
Hatutoi zaka kulingana na sheria ya Musa,
bali ni kulingana na ahadi za Mungu.

"Mdogo hubarikiwa na mkubwa" (**a.7**).

Melkizedeki alimbariki Ibrahimu na vivyo hivyo sisi kama wahudumu tunapoipokea zaka kwa ajili ya Yesu, tunabariki. Ni njia kuu sana naya nguvu kuomba zile baraka ambazo zimetajwa katika **Malaki 3,** tukiufwata mfano wa Melkizedeki Katika **Mwa.14**.

TUNAITIKIA AJE NENO LA ZAKA?

Maandiko ni wazi: **sehemu ya kumi ya yote ninayopokea ni ya Bwana**. Wakati wote ninapopata mshahara, malimbikizi, maongezeko, marupurupu, tunatakiwa kutenga sehemu ya kwanza ya kumi kwa Bwana kama zaka. Kwa maneno mengine tunatoa **zaka katika 'maongeo' ambayo Mungu ametupatia**, katika ulimwengu wa sasa, ni pesa au fedha, wala sio tena mazao ya kilimo na mifugo.

Zaka ni katika 'maongeo'

Wengine husema kuwa urithi tunaoupokea baada ya kifo cha mwenye mali hiyo hatustahili kuitolea zaka maana sio 'maongeo', bali ni **njia ya maongeo ya siku za usoni**. Vivyo hivyo baba anapoaga na kumpokeza biashara mmoja wa wana wake katika maisha yake, mrithi hastahili kutoa zaka ya udhamana wa biashara aliyopokea bali **atoe zaka kulingana na kile biashara inazalisha**. Hata hivyo ikiwa urithi ni katika pesa taslim au vitu ambavyo vyeweza kuuzwa basi maoni yangu ni kutoa zaka katika 'maongeo' yaliyopokelewa.

TUNAMTOLEA NANI ZAKA?

Tunafwata mfano wa baba yetu, Ibrahimu – alimtolea zaka Melkizedeki, ambaye alikuwa ufunuo wake Yesu Kristo Mwana wa Mungu. Kwa hivyo **tunamtolea zaka Bwana Yesu Kristo**. Unauliza, unawezaje kumtolea zaka Yesu hali humuoni? Hapa ndipo ufunuo unahitajika. Ibrahimu hangemuona Melkizedeki kimwili! Melkizedeki kulingana na **Ebr.7** ni kiumbe cha milele. Hata Yakobo alijitolea nadhiri ya kuwa mtu wa kutoa zaka, lakini alitoaje zaka kwa Mungu asiyemuona?

Zaka ni ufunguo wa kuishi kulingana na uchumi wa ufalme wa Mungu. Ufalme wake ni wa kiroho, unaotawaliwa na sheria za kiroho ambazo ni za kutegemewa na za manufaa kupita

mipaka ya kawaida. **Tunalipa zaka zetu kwa wale wanaotutunza kiroho, wachungaji na waalimu ambao wanatulisha kiroho,** ili wakaweze kuendelea kufanya kazi ya huduma ambayo Bwana amewapa kutekeleza.

ZAKA ZINATUMIWA KWA KAZI GANI?

Kulinga na Agano la Kale, zaka zilikuwa maongeo au urithi wa Walawi ambao kama kabila hawakuwa na urithi katika nchi. Kwa matendo, zaka hutumiwa **kuwasaidia wahudumu, wanaofunza, chunga na kulisha kundi la Mungu kiroho**. Wanaohudumu kiroho, wanatakiwa kusaidiwa katika mali ya asili. **1Tim.5:18** ***"Kwa maana andiko lasema, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Na tena mtenda kazi astahili ujira wake.'"***

1 Kor.9:11 "***Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini?***" **a. 14** "***Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio injili wapate riziki kwa hiyo injili."***

WAPE WAPENDWA NAFASI YA KUTOA

Kanisa linapoendelea kukua katika nyumba vyema, hata katika mikutano ya mara kwa mara, **wape wapendwa nafasi ya kutoa**. Kanisa la kibiblia la nyumbani halikujitenga, halikukosa uhusiano bali lilikuwa sehemu ya kanisa katika mji lililoongozwa na na kuhudumiwa na wazee wa mji. Huduma katika kanisa hilo ni ya mchungaji au wazee pamoja na wengine katika huduma tano za Efeso 4:11 wanapokuja katika mji. Katika Maandiko Matakatifu, mitume pamoja na wahuduma wengine walihudumu nyumba kwa nyumba. Kwa hivyo **mahali pa msingi pa kutoa zaka ni katika kanisa linalokutana iwe ni katika nyumba, ukumbi ama mahali pale ambapo pamewekwa wakfu kwa kanisa kukutana.**

Kulipia gharama za kanisa.

Gharama mbazo hutokea wakati wa mikutano ya kanisa ama kwa ajili ya muhudumu mgeni zinaweza kulipiwa kutoka kwa sadaka. Ila mchango wote unaotolewa unatakikana kuwekwa chini ya miguu ya mitume, au wazee wa mahali ikiwa wametambulika.

Kuajiri mchungaji

Wakati unapowadia wa kuajiri mchungaji [mzee aliyetawazwa] kwa malipo kidogo ama mshahara, hili linaweza kuongozwa na afisi ya mitume hadi kuwe na makanisa ya nyumba ya kutosha ambayo yataweza kufanya kazi kwa kujitegemea, yakiwa na wazee wao na wanatawala fedha zao wenyewe.

SHUHUDA

Ushuhuda wake Paul Galligan: wakati nilipokuwa mkristo mchanga, sikuwa na ajira, lakini nilikuwa nimepokea mshahara wa $400, ambao ulikuwa mashahara wa kazi niliyokuwa nime fanya awali. Niliweka hizo pesa kwenye benki, halafu nikaokoka. Baada ya siku chache **nikawa nimeshawishika moyoni kuwa sehemu ya kumi ni ya Mungu.** Nilikuwa sijapata mafunzo yo yote kuhusu zaka; hata nilikuwa sijasoma katika Maandiko; asili yangu ya kikatuliki haikuwa imenifunza juu ya zaka. **Huu ulikuwa ni ufunuo kutoka kwa Mungu.** Nikaondoka kuelekea kwenye benki kutoa $40 ambayo ni ya Bwana na wakati huu sikuwa mshirika wa kanisa lo lote. Njiani nikaokota kijikaratasi ambacho kilizungumzia juu ya 'Uinjilisti wa kisiri' katika Ulaya ya Mashariki. Huu ulikuwa mwaka wa 1974. Nikaingia kwenye benki na kuandika hundi ya pesa kwa ajili ya 'Uinjilisti wa Kisiri'.

Zaka na ukame

Mwisho mwisho wa 2002 nilipokea mafundisho kutoka kwa mtume John Alley juu ya zaka na ukame. Mafundisho hayo **yalifananisha ukame kuwa ni sababu ya watu kukosa**

kumtolea Mungu zaka. Mungu aliahidi katika **Mal.3:10b** kuwa tukileta zaka kamili 'ghalani' ndipo atakapofungua ***'madirisha ya mbinguni***,' ni kusema, atume mvua inayohitajika katika ulimwengu wa asili. Tulipata changamoto kutokana na mafundisho haya **tukaanza kuhakikisha kuwa zaka yetu inatolewa kwa wakati unaofaa**.

Kama huduma sisi huhakikisha tunatoa zaka kutoka kwa maongeo yote tunayopata. Tulikuwa na kiasi cha pesa katika akaunti yetu ya zaka na kuandika hundi ya pesa na kumtolea Bwana jinsi anavyo tuongoza. Baada ya kuandika hiyo hundi ya pesa na kukusudia mioyoni mwetu ni wapi tutapeleka, wengine wetu tuliokuwa afisini **tuliomba kwa Bwana kutulipa kulingana na Neno Lake tukiamini kuwa atatuma mvua nyingi inayohitajika katika nchi yetu.** Tulipokuwa tukiomba, Bwana akajidhihirisha kwetu katika njia kuu na Mungu akatupatia **maono ya Melkizedeki, mfalme na kuhani**, akiwa amesimama afisini mwetu **kupokea zaka yetu**. Sote tukapiga magoti mbele yake na kunyenyekea kwa ajili ya thibitisho hili la ajabu la utiifu kwa Neno Lake. Baada ya miezi mingi watu wangekuja kwetu na kutoa zaka zao na kutuuliza kuombea mahitaji ya kumaliza ukame katika maeneo yao. Katika kila hali tuliyoombea, **mvua ilinyesha** katika majuma mawili, sehemu zingine hata baada ya siku mbili; sehemu zingine walipokea mvua kati ya [150-225mm], ikijaza mabwawa na kuzalisha mashamba.

TENDO LA HAKIKA

Katika jumuia yetu, watu hupata fursa kila jumapili **kuweka zaka zao katika mfuko wa sadaka**. Tumetengeneza bahasha mbali mbali ili watu waweze kutofautisha kati ya zaka na matoleo ya kawaida. Hili linatusaidia kuweza kuwajibika zaidi kwa jinsi ya kutumia zaka. Watu wengine huamua kuja afisini katika juma na **kutoa zaka zao binafsi**. Wakati watu wanapofanya hivyo, sisi huchukua wakati na kuomba baraka kulingana na **Mal.3:10-12**.

Pia sisi **hupokea zaka kwa njia ya barua** kutoka kwa watu ambao wanakaa mbali nasi. Tunapoyatembelea **makanisa ya maeneo yetu**, **wapendwa mara nyingi hututolea zaka zao.** Tunapokea na kutambua zaka zote tunazopokea binafsi. Tunapopewa sadaka ya kawaida pia huwa tunaipokea kama kawaida.

Tunawaombea wale ambao wanatoa zaka zao na kutoa kwa ajili ya huduma katika njia yo yote ile.

Tunawahimiza watu kutoa zaka zao na sadaka wakikusudia.

Tunawahimiza watu kupanga kutoa, na kulifanya kuwa jambo la muhimu katika jamii.

Tunahitaji kuyajua Maandiko yanayozungumzia kutoa zaka na kumuamini Mungu kwa ajili ya ahadi kuzitimiza.

ZAKA KATIKA ZAKA

Walawi walitoa zaka kwa jamii ya kuhani mkuu

Katika **Hes.18:25-28** tuna soma juu ya maagizo ya Mungu kuwahusu Walawi. Mtakapoitwaa zaka mkononi mwenu tenga zaka [sehemu ya kumi], kama sadaka ya kusongeza juu kwa BWANA katika hiyo. ***"Tena utanena na Walawi, na kuwaambia, hapo mtakapoitwaa zaka mkononi, mwa Wana wa Israeli niliyowapa ninyi kutoka kwao kuwa urithi wenu, ndipo mtakaposongeza sadaka ya kuinuliwa kwa BWANA katika hiyo, iwe zaka katika hiyo zaka.'"*** **a.26**. Zaka katika zaka ilikuwa ipewe Haruni, kuhani mkuu na nyumba yake.

"Hivyo ninyi nanyi mtasongeza sadaka ya kuinuliwa kwa BWANA katika zaka zenu zote, mpokeazo mikononi mwa wana wa Israeli; kwa hiyo mtampa Haruni kuhani hiyo sadaka ya kuinuliwa kwa BWANA." **a.28**. Walawi walipokwa zaka, lakini pia walimtolea Haruni kuhani mkuu zaka. Zaka katika zaka ilitumwa kutoka maeneo mengine kwa hekalu la Yerusalamu, **Neh.10:38-39** ***"… nao Walawi watapandisha zaka ya hizo zaka nyumbani***

kwa Mungu wetu, vyumbani, katika nyumba ya hazina.... wala sisi hatutaiacha nyumba ya Mungu wetu."

Huduma na makanisa yanatoa kutoka kwa kila mapato
Huduma ya uvuvio ya Australia tangu kuanzishwa kwake Januari 1998, imekuwa siku zote ikitoa zaka kutoka kwa kila mapokezi. Tunaandaa 'zaka katika zaka' tunapokuwa tunaweka pesa kwenye benki, na hizi pesa hazitumiwi kwa jambo lingine lo lote. **Kutoka kwa hazina ya 'zaka katika zaka' tunasaidia huduma zingine kama vile Bwana anavyotuongoza.** Katika miaka hizo, zaidi tumekuwa tukiwasaidia wachungaji na mitume katika nchi zinazoendelea lakini hapa kwetu Australia tunabariki huduma ambazo hazijakuwa na msingi wa kanisa wa kupokea zaka na sadaka kutoka kwa washirika. Hivi karibuni, mtume John Alley amekuwa muangalizi wetu wa kiroho na baba katika Bwana na sasa tunaunga mkono huduma yake ya utume katika mataifa kutoka kwenye hii hazina.

Bwana anawaheshimu wale ambao wanamtolea kwa uaminifu
Bwana ametuheshimu kwa jinsi ya kuwa waaminifu katika zaka kutoka kwa mapato yetu yote. Tunaomba kila mwezi jinsi ambavyo tutaweza kutumia zaka na Bwana ametuongoza wazi jinsi ya kufanya hivyo. Ametuweka kuwa watu waliowajibika katika huduma ya zaka. Mapato yetu ya huduma kidogo yamekua na kila wakati tunawezeshwa kukutana na mahitaji yetu ya kifedha ambayo tunasikia kutekeleza.

ZAKA NI TOFAUTI NA SADAKA

Sadaka ni kupanda, kile unatoa kutokana na kile ulichobakisha baada ya kutoa zaka.

Toeni kama wapanzi mkitarajia mavuno.
Kuwa wazi kuhusu mbegu unayopanda, ukijua kiwango cha mavuno ambacho hiyo mbegu itazalisha.
Kisha jiandae kwa mavuno!
Kupanda ni jambo moja, kuvuna ni kitu kingine!
Zinahitaji maombi na maandalizi na matendo!

Baraka ya kutoa na kupokea huenda sambamba na kuujenga uhusiano wa karibu na Mungu. Kumbuka Yeye ni Bwana wa Mavuno! Hatupotezi sadaka, kwa sababu sadaka **ni mbegu**. Mkulima huwa hapeani mbegu yake; yeye huipanda. Wakati wote tunapotoa sadaka, hatuipotezi; bali tunapanda, tukitarajia mavuno.

Kazi ya sadaka ni nini?
Zaka ni za huduma! Sadaka ni ya mambo yale mengine, kama kodi ya nyumba, umeme na gharama zingine za mjengo. Makanisa hukosea wakati ambapo wanajiingiza katika madeni kwa ajili ya jengo kisha wanatumia mapato ya zaka kulipia hizo gharama, hiyo ni kudunisha **huduma ya Neno**. Matokeo ni: watu wanaanza kusema kuwa haja ya kanisa ni pesa tu. Hawautafuti ufalme wa Mungu kwanza.

Mungu anatwambia wazi katika Neno Lake kuwa **tutoe zaka**. Neno la Mungu pia linazungumzia **sadaka mbali mbali**. Mojawapo ya sadaka ambayo Bwana aliamuru ilikuwa ni ya kujenga Hema ya kukutana jangwani. Hata hivyo, watu walitoa kwa moyo mkunjufu hadi Musa akawasihi waache kutoa zaidi. Kile kilichotolewa kwa ajili ya ujenzi wa Hekalu kilitolewa kwa wingi na Mfalme Daudi kutoka kwa hazina yake ya mfalme. Hizi **ni baadhi ya mifano ya sadaka kwa ajili ya mjengo**. Katika Agano Jipya kanisa la Yerusalemu liliuliza sadaka kwa ajili ya watu masikini. Paulo mtume akaongoza mchango mkubwa kutoka kwa makanisa yote ambayo alikuwa amehubiria. Hii ilikuwa **sadaka maalum kwa ajili ya maskini**.

SADAKA NI YA HIARI.

Wakati mwingine katika mikutano ya kanisa, watu wanasukumwa kutoa**. Hivi si vyema. Wapendwa wanatakikana wafundishwe na kuelekezwa kuhusu kutoa. Mfano wa Biblia ni kutangaza mapema kisha kuipokea baadaye.**

Hudson Taylor wa Misheni ya Ndani ya Uchina, ambaye binafsi aliwasadia wamishonari 100 ndani ya Uchina, hakuruhu kanisa lo lote huko Wingereza kupokea sadaka baada yake kuhubiri. Badala yake aliwashauri watu kuwa, kama Mungu ameweka ndani ya moyo wako kuchanga kwa ajili ya huduma yake, enda nyumbani na utume hundi ya pesa siku inayofuata. George Mueller ambaye alianzisha nyumba nyingi za yatima katika Wingereza aliishi maisha ya imani kuhusu fedha. Hakusema juu ya mahitaji yake ila kwa ushirika mdogo wa maombi ambao pia walimuamini Mungu. Tabia ya kuwasukuma watu kutoa katika mkutano sio njia ya Mungu.

SADAKA MBALI MBALI

Watu wengine husema kuwa, 'sina uwezo wa kutoa zaka!" wanasema kinyume na Maandiko Matakatifu. **Wakati tunapotoa zaka zetu, Mungu huyashughulikia mahitaji yetu yote**. Kutoa zaka ni njia ya matendo ya ***"kuutafuta ufalme wa mbinguni kwanza"*** katika msingi wa **Matt.6:25-34**. Hata hivyo, **sadaka ni kwa hiari,** hivyo ni kusema**, ni uamuzi wa yule anayetoa kile ambacho anataka kumtolea Mungu**. Wateule wengine hutoa sadaka yao mara kwa mara zaidi ya fungu lao la kumi kwa kanisa. Wakati mwingine, watu hutoa **sadaka ya kuwabariki wahudumu wageni, misheni, wanalipa kodi ya nyumba au hitaji lingine lo lote.** Wakati mwingine mtu anataka kutoa lakini hana uhuru kulingana na bajeti yake. Hii ni nafasi nzuri ya **kuiweka imani katika matendo na kumuuliza Mungu kwa ajili ya sadaka**. Ana ng'ombe katika milima elfu na anauwezo kupeana sadaka ili uweze kumtolea. Jichunge na kupeana bajeti ya chakula cha familia yako! Watoto wako hawatafurahia 'mkate kavu' kwa wiki nzima. **Tunashauri kuwa kila jamii ijipange jinsi ya kutoa**. Tayari tumesema kuwa watu wasilazimishwe kutoa katika mikutano; bali **mfano wa Biblia ni kutangaza mapema halafu kuipokea baadaye.** Kwa hivyo jamii yote ikiwa imekubaliana kutoa kupita kiwango chao kwa sababu Mungu amewazungumzia, **watauona utukufu wa Mungu.**

TAMATI

Mafundisho juu ya zaka na sadaka ni ya msingi. Wakati kanisa linapokuwa linaendelea vizuri, kulingana na mfano wa Neno la Mungu, katika maeneo ya kutoa, hilo kanisa litabarikiwa. Ushuhuda wetu ni kuendela kubarikiwa ambapo tunamshukuru Mungu kila siku. Siku hisi tunasema kuwa **kabla tumuombe Mungu amesikia na wakati tunapokuwa bado tuna nena tayari ametuma jibu** (**Isa.65:24**).

Sifa ni kwa Jina Lake Takatifu!

Toa zaka katika matarajio kuwa Mungu atatimiza ahadi zake zote!
Kuna Baraka kwa ajili ya wote wanaotoa zaka zao!
Panda sadaka yako na utarajie mavuno!

SURA YA NNE

KUSUDI NA MWENENDO WA HUDUMA KATIKA NYUMBA

UTANGULIZI

Kanisa katika Agano Jipya ni kanisa linalokutana katika nyumba. Mitume walifundisha mafunzo ya Kristo katika mikutano ya nyumba walipokuwa wakikutana kila siku. Kulikuwa na mikutano ya nje lakini zaidi ilikuwa ya uinjilisti na kwa hivyo kulihitajika ukumbi kama jinsi ya Paulo kule Efeso ambako aliwakusanya wanafunzi, lakini hapakuwa na 'ukumbi wo wote uliokuwa umewekwa wakfu kuwa kanisa.' Katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na urejesho wa huduma ndani ya nyumba, kutoka kwa vikundi vidogo vidogo miaka ya 1970 kwa vikundi vya makanisa miaka ya 1990. Pamoja na hayo, kumekuwa na majaribio ya kanisa katika nyumba kulingana na Agano Jipya.

Chakula cha Bwana, ndicho kiungo muhimu katika kanisa la nyumba

Kuna mambo mengi yanayolenga "kanisa katika nyumba", lakini kiungo muhimu ni Meza ya Bwana. Kihistoria, 'meza' za madhehebu zimefanywa kuwatenga watu wengine na kufunika mambo ambayo wamejitungia kuwa siri na kuamriwa kulingana na mashrti makali ya dhehebu. **Ni ushindi mkuu wakati wapendwa wanaposhiriki Meza katika ushirika wa kawaida ambao unadhihirisha kuthibitisha matendo ya Kanisa la Agano Jipya.** Katika njia ya kweli, **kumega mkate kunadhihirisha kuimarika kwa kanisa**. Ulimwenguni kote, makanisa ya nyumba yenye ushawishi wo wote, yakiwa sehemu ya dhehebu lo lote au muondoko hayaruhusiwi kumega mkate katika nyumba. Kumega mkate ni jambo ambalo limetengewa mikutano ya hadhara ya kanisa. Kwa hivyo hakuna kutambulika kwa kanisa la nyumba kama sehemu ya msingi katika tendo la biblia ambalo haliruhusiwi.

KODESHA UKUMBI, MATANGAZO, WAZI!

Kama kanisa ambalo linakutana nyumbani lilipokuwa linaanza kunawiri, nilijiunga na dhehebu la kikarismata na kujifunza njia zao za kupanda makanisa mapya. Hii ilimaanisha kukodesha ukumbi wa kijamii, nifanye matangazo, na mabango ya vitambaa yaliyokuwa na jina la kanisa letu na kadhalika, na hii **ilimaanisha kuachana na ushirika wa kweli ambao ulikuwa ukiendelea katika kanisa la nyumba.**

VIKUNDI VYA NYUMBA

Makanisa mengi husisitiza kuwa na "*vikundi vya nyumba****"*** lakini vikundi hivi, havielezei makusudi na mwenendo wake. Swali ni Je! Vikundi hivi huwa ni sehemu ya kanisa ambayo imesambazwa hadi manyumbani? Je! Nia yake ilikuwa nini, kujenga uhusiano na kukua kiroho kupitia kwa vikundi vidogo vidogo? **Je! Vilikuwa vikundi kulingana na Maandiko jinsi ushirika wa kanisa kuliko mkusanyiko mkubwa wa dhehebu?**

Maswali haya hayakujibiwa ipasavyo kwa sababu hapakuwa na kiongozi wa kiutume ambaye aliweza **kufundisha kwa ufasaha kutoka kwa Maandiko Matakatifu jinsi kanisa la kweli linavyostahili kuendeshwa siku baada ya siku na nyumba kwa nyumba.** Tulitafuta ushauri kutoka kwa wengi lakini maoni mengi bila ya muongozo uliokuwa unafaa tuliupata.

VIKUNDI VYA MAKANISA

Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na vikundi vya makanisa na vikundi mbali mbali ambavyo vimechipuka kulingana na mifumo ya aina fulani katika kuendesha mikutano yao.

Pia katika vikundi hivi, hapakuwa na muongozo wa kiutume kwa namna vinaweza kuufikia utimilifu katika Yesu Kristo. Kuna sheria nyingi na maelezo mengi kuhusu jinsi ambavyo mambo yanavyostahili kuendeshwa. Kwa hivyo mtu anaweza kuuliza, 'Je! Huu ni mfumo mwingine tu wa kanisa?' naogopa ni kweli.

UREJESHO WA KANISA NDANI YA NYUMBA

Katika mapana, **vikundi vingi vidogo vimefaulu katika kutoa malezi bora ya uchungaji na ushirika kwa wateule,** lakini mara nyingi **hushindwa kuwaleta wapendwa na kuwaonyesha huduma na jinsi ya kutumia vipawa katika utenda kazi katika Mwili wa Kristo.** Hii ni kwa sababu bado kuna **ufahamu wa msingi juu ya kanisa la nyumba ambao unakosekana!**

Kulingana na Maandiko Matakatifu katika Agano Jipya kanisa la nyumba ni kanisa la msingi ambalo linaendelea.

Mifano ya kanisa ambalo linatiwa nguvu na vikundi vidogo vidogo sio Agano Jipya. **Mikutano ya kweli ya nyumba kwa nyumba ya wateule ndilo kanisa la pekee linalopatiana katika Agano jipya** ila kwa mahubiri ya wazi na ushuhuda mahali kama Ukumbi wa Suleimani (**Matendo 5:12**), na shule za mafunzo za utume kama shule ya Tirano kule Efeso (**Matendo 19:10-11**).

KUSUDI LA KANISA KATIKA NYUMBA

Kusema ukweli: **kusudi la kanisa ndani ya nyumba ni :**

1. kupanda makanisa ya Kibiblia
2. kulituma kutenda kazi.

Hii ni aina ya huduma ambayo Yesu aliwapa wale mashahidi sabini katika **Luka 10**: walitakikana kukaa katika nyumba ya mtu wa amani [nyumba ya rafiki, nyumba ambayo wanapokewa], ponya wagonjwa na hubiri ufalme wa Mungu. Hawakutakiwa kwenda nyumba hadi nyumba bali matarajio ya Yesu yalikuwa kwamba **wagonjwa na waliopotea watavutwa kwenye nyumba ambayo wahudumu wa injili walikuwa** (**Lu.10:1-9**).

KANISA NDANI YA NYUMBA KATIKA MATENDO YA MITUME

Kuna mifano mingi katika kitabu cha **Matendo** kuhusu kanisa ndani ya nyumba:
Matendo 1:12-26 wale mia na ishirini walikuwa pamoja wakingojea katika chumba cha juu, wakiendelea katika maombi mpaka Roho Mtakatifu Akaja – **walikuwa ndani ya nyumba.** Ni katika muda wa haya **maombi na dua,** ndipo mtume yule wa kumi na mbili, wa kuchukuwa mahali pa Yuda, alichaguliwa. Hakika **Maandiko yalikuwa wazi** katika mkutano huu wa nyumba na **Roho Mtakatifu akanena** na Petro kupitia kwa Maandiko.

Matendo 2:42-47 baada ya mahubiri ya wazi barabarani Siku ya Pentekoste, watu elfu tatu walibatizwa na wakajumuishwa na wale mia na ishirini. **A.42** ***"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."*** Je! hao 3120 walidumu wapi? Walikuwa wakikutana wapi? Hili ni swali la maana sana ambalo watu wengi hawaulizi au pia kupuuza jawabu. **V.46** ***"Walidumu ndani ya hekalu …, wakimega mkate nyumba kwa nyumba."*** **Walikutanika katika nyumba kadha.** Unaweza kufikiria kuwa chumba cha juu katika **Matendo 1** labda kilihifadhi wengi kidogo kupita wale 120. Wapendwa wale wengine walifungua milango ya nyumba zoa, wakiwakaribisha wale waliokuwa wameokoka na wamebatizwa na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu siku waliyo amini, kuja katika **mikutano ya nyumba mahali ambapo mitume walikuwa wakifundisha kila siku**. Pamoja na hayo, kulikuwa na maombi ya kila siku katika maeneo ya hekalu, kama ukumbi wa Sulaimani katika (**Matendo 5:12**).

Matendo 4:23,31 baada ya Petro na Yohana kufunguliwa ***"wakaenda kwa watu wao"***, [tunaweza kusema kuwa walienda kwa nyumba fulani] na wakamuomba Mungu kuhusu hali yao na kuomba Bwana ujasiri na ishara na ajabu nyingi. ***"Hata walipokwisha kumuomba Mungu mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri."***

Matendo 5:42 ***"Na kila siku ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo."***

Matendo 9:11-19 Sauli alikuwa ***"katika nyumba ya Yuda katika njia iitwayo Nyofu"***. Paulo aliponywa, akajazwa na Roho Mtakatifu na akabatizwa na Anania ndani ya Nyumba.
A.33-34 Petro alimponya mtu aliyekuwa amepooza **kutoka kitandani mwake** – tunafikiria lazima hapa ni ndani ya nyumba.

Matendo 10:24-48 Kornelio **aliwakusanya watu wakwao wote na marafiki katika nyumba yake kumsikiza Petro akishiriki ujumbe wa Yesu Kristo**. **A.44** ***"Petro alipokuwa akinena mambo hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile Neno"***. Petro akamuru wabatizwe [lazima walikuwa na maji ndani ya nyumba – labda kuoga kwa Kirumi!] na **akakaa nao kwa siku chache akiwahudumia.**

Matendo 12:12 wakati malaika alipomuokoa Petro kutoka gerezani alienda kwa **nyumba ya Yohana Marko** ***"watu wengi walikuwa wamekutana humo wakiomba"***.

Matendo 16:15-40 Lidia aliokoka kupitia kwa mahubiri ya Paulo na mara alipobatizwa alimsihi Paulo na kikundi chake ***"waje nyumbani mwake na wakae"***. **Kanisa la huko Filipi lilipandwa katika nyumba ya Lidia**. Humo ndimo kanisa lilikutanika. Wakati Paulo na Sila walipoachiliwa kutoka gerezani walirudi katika nyumba ya Lidia ambako waliwaona wapendwa (**a.40**). Katika **a.33-34**, askari wa magereza na nyumba yake wote waliokoka na mara moja wakabatizwa; kisha akawaleta mitume katika nyumba yake na kuandika chakula mezani kwa ajili yao. Pia mwenendo na kusudi la uhai wa kanisa ulikuwa katika nyumba.

Matendo 18:7 katika Korintho, Paulo awali alikuwa amewashuhudia Wayahudi katika Sinagogi lakini upinzani ulipoinuka, ***"Akaondoka huko akaenda kwa nyumba ya mtu mmoja aitwaye Tito Yusto, mcha Mungu ambaye nyumba yake ilikuwa mpaka mmoja na Sinagogi."***
a.8 ***"Na Krispo, mkuu wa Sinagogi, akamwamini Bwana pamoja na nyumba yake yote."*** Mara nyingi katika Agano Jipya **uinjilisti ulifikia nyumba yote**; hii ni kwa **sababu huduma ya injili ilikuja katika nyumba!**

Matendo 20:20 Paulo anashuhudia kuwa kule Efeso ***"aliwafundisha wazi wazi na nyumba kwa nyumba"***. Alikuwa akinena mbele ya wazee kutoka kwa kanisa la Efeso. Wakati Paulo alipokuwa Efeso alifundisha wazi wazi, kila siku katika shule ya Tirano. Bali kanisa lilikutana katika nyumba na kwa hivyo jioni Paulo alihudumu kutoka nyumba hadi nyumba. Mfano wa Shule ya Tirano ndio mfano wa shule za utume.

Matendo 21:8 Wakati Paulo na wenzake walipofika Kaisaria, "***aliingia katika nyumba ya Filipo Muhubiri wa injili, aliyekuwa mmoja wa wale saba, tukakaa kwake."*** Mikutano ya nyumba ilifanyika kwa makusudi na baada ya siku nyingi Agapa nabii akawasili kutoka Uyahudi na akahudumu katika nyumba (**a.10-14**).

Matendo 28:30-31 ***"Paulo akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake ambayo alikuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuwafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu."*** Paulo alifundisha miaka miwili katika shule ya Utume huko Efeso, na alijitolea katika funzo la mitume katika nyumba aliyoipanga mwenyewe kwa miaka miwili. Hii ni picha ya mwisho ya mtume mkuu Paulo katika Maandiko na **anahudumia kanisa ndani ya nyumba**.

Tumeangalia maandiko yanayolenga mikutano katika nyumba moja kwa moja na jinsi yalivyo endeshwa katika kitabu cha **Matendo**. Kuna Maandiko mengine mengi ambayo hayalengi moja kwa moja kwa sababu

> **Mikutano mingine yote na kuendeshwa kwa uhai wa kanisa kutoka kwa wokovu pamoja na ubatizo hadi hekima iliyokuu ya Neno la Mungu iliyokuwa ikifundishwa na mitume, ilifanywa nyumba kwa nyumba.**

HUDUMA YA NYUMBA KATIKA NYARAKA

Rum.16:5 ***"Pia lisalimieni kanisa katika nyumba yao*** [Priska na Akila]***"***
a.10 ***"Nisalimieni wale wa nyumba ya Aristobula".***
a.11 ***"Nisalimieni watu wa nyumba ya Narkiso walio katika Bwana."***
a.14 ***"Nisalimieni Asinkrito … pamoja na ndugu walio pamoja nao."***
a.15 kikundi kingine cha wapendwa kilikuwa na wapendwa ambao Paulo aliwajua kwa majina. Paulo wakati anaandika waraka huu alikuwa hajawahi kwenda Roma lakini anajua ***'wapendwa katika nyumba kadhaa'***, ***'kanisa katika nyuma'***, ***'wandugu pamoja'***. Kuna vikundi vitano vya aina hii na ni mawazo mema kuamini kuwa kulikuwa na shirika tano za nyumba ambazo zilikuwa sehemu ya kanisa kule Roma.

1 Kor.16:15 inazungumzia juu ya **nyumba ya Stefana** walio ***"jitia katika kazi ya kuwahudumu watakatifu"***. Stefana anatajwa kama muhudumu na mtenda kazi pamoja na Paulo. Alihudumu kupitia kwa kanisa lililokuwa katika nyumba yake pamoja na kusafiri katika huduma.
a.19 Priska na Akila walikuwa na **kanisa katika nyumba yao** kule Efeso, na pia kule Roma kisha mapema baadaye kule Korintho.
Kol. 4:15 hapa kanisa limo **nyumbani mwa Nimfa**
Filemoni 1-2 Filemoni alikuwa mwenyeji na kiongozi wa kanisa ndani ya nyumba yake.
a. 4-6 Alijulikana kwa upendo wake na imani na huduma ya kuwaburudisha wapendwa na hata Paulo Mtume, **20-22**.

Kama katika **Matendo** kuna baadhi ya Maandiko ambayo yanalenga moja kwa moja kanisa katika nyumba. Hata hivyo, hakuna mahali po pote katika kitabu cha **Matendo** au katika **Nyaraka** kuhusu kanisa kukutana mahali pengine. **Ni wakati wa kurudia Ukristo wa Agano Jipya, tufuate mfano wa mitume ambao uko wazi katika Maandiko matakatifu.**

KAMA ILIVYOANDIKWA

Mitume katika Biblia wanahudumu wazi wazi na nyumba kwa nyumba. Huduma wazi ilikuwa ni uinjilisti, lakini pia ilihuzisha kunena katika hekalu mara kwa mara katika miaka ya kwanza ya kanisa na pia maeneo ya Hekalu. Hata hivyo, **uhai wa kanisa la Agano Jipya ulikuwa katika nyumba**. Wakristo wachanga alipoondoka kwenye mikutano ya nje walipokelewa katika kanisa; kanisa lile lililokutana katika nyumba. Wale elfu tatu walio okoka Siku ya Pentekoste walijiunga pamoja na wale mia na ishirini na walikuwa wakikutana

kila siku, na walikua kila siku ***"Bwana akiongeza wale waliokuwa wakiokoka kia siku"*** **Matendo 2:47**.

Mahali pa pekee ambapo pametajwa kuwa mahali pa mkutano wa kanisa katika Maandiko ni katika nyumba. Ndio! Ushuhuda wazi ulifanyika katika sehemu mbali mbali, lakini hakuna mahali ambapo Biblia inatwambia kuwa kanisa lilikutana mahali hapa au pale kuendesha kanisa. Kwa nini, basi kuna hali ya kutatanisha siku hizi? Mara nyingi nikiwaambia wahudumu jinsi ya kuanzisha huduma ndani ya nyumba, jibu huwa, *'Aha! kikundi kitakapo kua, tutaweza kupata jengo.'* La! Hilo sio lengo letu.

Lengo ni kuongezeka kwa wanafunzi wanaokutana katika nyumba
Kusikiza mafunzo ya mitume,
Kushiriki pamoja, pamoja na kukutana na mahitaji ya wengine,
Kumega mkate wakati wote – kila siku
Na kusali pamoja kutambua kusudi la Mungu siku baada ya siku
Kuwatunza wachanga kiroho
Kuwafanya wanafunzi.

WALE MAELFU WALIOOKOKA WALIKUTANIA WAPI?
Je! Ushawahi kuuliza: *'Ni nini kiliwatendekea 3000 waliookoka katika* ***Matendo 2:41****?' 'Ni nini kiliwatendekea wale 5000 katika* ***Matendos 4:4****?' Ni nini kiliwatendekea wale waliokuwa wakiongezeka kila siku kwa kanisa?* ***Matendo 2:47****'*. Wale kutoka **Matendo 2:47** walijiunga na makanisa ya nyumba; lakini wale 3000 na 5000? Walihudhuria kanisa wapi? Jawabu la pekee ni: **katika nyumba za waaminio au labda katika nyumba zao wenyewe.** Hakika tunaweza kusema kuwa kanisa liliendelea kukutana katika nyumba ya Kornelio katika **Matendo 10.** Tunaweza kuona kanisa likiendeshwa katika nyumba ya askari wa magereza huko Filipi baada yake na nyumba yake kuokoka. Ni wazi kuwa Lidia aliwakaribisha Paulo na wandugu kwa nyumba yake kama kanisa mpya katika Filipi.

ACHA KWENDA KANISANI!
Sio hatua ya kuendelea ikiwa wapendwa watakutana nyumbani kisha ushirika unapokua, wanatafuta mjengo kwa ajili ya kusanyiko. Hakika hilo linapotendeka, tunakuwa tumerudi nyuma na litakosa kuimarika jinsi ambavyo Mungu alivyoliteua. Kusema kuwa kanisa ni kusanyiko linalokutana kila jumapili sio hakika ya mfano ambao Biblia imepeana, na pia sio njia ya kufanya wanafunzi.

ANZA KUWA KANISA!
Ni mabadiliko katika Ukristiano kutambua kuwa 'tuache kwenda kanisani' na 'kuanza kuwa kanisa'.

KUENDESHA KANISA LA NYUMBA

1. **Kupitia kwa maombi, kuwezesha waliopotea kumpata Yesu**
2. **Sifa na Ibada**
3. **Ushirika na kushiriki**
4. **Mafunzo ya mitume – kuongoza mafunzo yaliyo hai, ufunuo unafahamika na neema inapokelewa.**
5. **Nafasi nyingi za huduma – ishara na maajabu, kuhubiri na kufundisha.**

Matendo 2:42 ***"wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."*** Huduma katika utano ilifanyika katika nyumba. Mitume walikuja nyumbani na kufundisha; wapendwa wakashirikiana; wakamega mkate na

kuomba pamoja. Mambo hayo manne ni nguzo katika kanisa la nyumba. Hata utapata watu waliokomaa siku zote wakitegemea watu fulani kanisani – maana hawajapata nafasi ya kuhudumu nyumbani, kila siku, wakimega mkate, kusali na kusoma Neno la Mungu.

a.43 ***"kila mtu akaingiwa na hofu; maajabu na ishara nyingi zikafanywa na mitume"*** kuna ushahidi wa ufalme wa Mungu miongoni mwao. Wagonjwa walipona; miujiza ilikuwa ikitendeka nyumbani.

a.44-45 ***"Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika. Wakauza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja."*** Ushirika unaotokana na huduma nyumbani huongoza kuwa na ushirika wa ndani sana. Kila mshirika anajulikana na anadhaminiwa; mahitaji binafsi yanashughulikiwa na kuombewa, na upaji unatoka kwa Mungu jinsi anavyoongoza.

a.46 ***"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe."*** Kulikuwa na nafasi kwa wandugu kukutana kila siku katika njia ya kirafiki, kushiriki chakula pamoja na kushiriki nafasi yao katika Bwana kupitia kumega mkate.

a.47 ***"Wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu wote. Bwana akilizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."*** Mahali pa sifa na ibada ni katika nyumba. Kanisa la nyumba ni la 'asili' katika kuwahudumia majirani na wote wanaoishi katika mazingara hayo ya kanisa. Wakristo wa kwanza '***waliwapendeza watu wote'*** – inamaanisha walijulikana. Majirani kwa wepesi wanaweza kujiunga na kanisa la nyumba.

USHUHUDA WA MAANDIKO NI DHAHIRI

Kanisa katika Agano Jipya lilikutana katika nyumba. Kanisa lilipandwa katika nyumba ya mtu wa amani. **Matendo 5:42** ***"Kila siku katika hekalu na kila nyumba, hawakukoma kuhubiri na kufundisha kuwa Yesu ni Kristo."*** Katika **Luka 10**, Yesu aliwatuma mashahidi wawili wawili katika mji na mahali ambapo alikusudia mwenyewe kwenda. Aliwaagiza kutafuta nyumba ambayo watakaribishwa wahudumu kutoka hapo, waponye wagonjwa, wahubiri ufalme wa Mungu.

LENGO NI KUPANDA MAKANISA MENGI

Lengo ni kuwa na kanisa katika kila nyumba ya mpendwa,
Kanisa katika kila orofa ya jengo
Kanisa katika kila barabara,
Kanisa katika kila eneo la kazi.

Ili injili ihubiriwe kikamilifu,
Ili tume kuu iafikiwe na kutimizwa,
Ili kanisa lijiandae kwa kurudi kwake Yesu,

Kunahitajika kanisa linalo ongozwa na Maandiko, linalookoa, ambalo limejaa Roho Mtakatifu miongoni mwa watu wake ili kila nafsi ifikiwe na iguzwe na Injili ya Yesu Kristo.

SURA YA TANO

PIGA TARUMBETA KATIKA SAYUNI
PIGIA MBIU FUNDISHO LA MITUME

KULINGANA NA MFANO WA MAANDIKO MATAKATIFU

Kupigia mbiu fundisho la mitume ni kuita kanisa kurudia mfano wa Maandiko na kutenda na kuliita lirudie Ukristo wa kiutume. **Kanisa lililobadilika** ni kanisa ambalo limerudia muundo, mpango wa Agano Jipya**,** kwa mfano**, 1Kor.12:28** yasema kuwa ***"Mungu amewaweka kanisani kwanza mitume, pili manabii, na tatu waalimu; baada ya hayo …"*** huduma zingine. Kwa hivyo tunahitaji mitume leo kuliongoza kanisa na kulirudisha katika mpango wa biblia na lihudumu humo. Mfano wa pili wa nguvu ni **Efe.4:7-16** ambapo tunasoma kuwa kanisa haliwezi kufikia utimilifu pasipo huduma tano **kufanya kazi. Kanisa lililobadilika ni lile ambalo** karama zote na huduma za Agano Jipya zinafanya kazi kikamilifu, **ambapo mbinu na ujanja wa mawazo ya mwanadamu hayajashamiri.**

KURUDI KWENYE MAANDIKO

Changamoto ya **Ukristo wa utume, ni kurudi kwenye Maandiko;** yaweza kuonekana kuwa gumu, la kusumbua na tena kinyume na yale ambayo watu wanaona kuwa matendo mema ya ukristiano katika makanisa ya kisasa na katika vizazi. Hata washirika wa kanisa la Musa walisikia hivyo kuhusu Kristo. Mafundisho yake na njia zake zilikuwa za ajabu na badala ya kupokea ufunuo ambao alikuwa akiwaleta, viongozi wa kanisa la Musa walimuona kama tishio kwa dini yao, utaratibu wao na njia ya kumtumikia Mungu. Walishindwa kuona kuwa

Yesu alikuja kuitimiza torati na unabii;
Yesu alikuwa kifaa kilichotumiwa kuuleta ukweli kutoka kwa mifano;
Ndani ya Kristo yote ambayo Mungu alifunua yanatimia sasa
Na yatathihirika katika kanisa la Yesu Kristo.

CHUNGUZA MAANDIKO

Wakristo wengi ambao wamejitolea leo wanapinga urejesho wa huduma ya utume. Viongozi wengi wananena kinyume cha mafundisho ya mitume bila hata kuchunguza kwa makini Maandiko, kuona ***"kama mambo haya ni kweli"*** **Matendo17:11.** Hata hivyo, Mungu anaendelea kuinua mitume na manabii ambao wanazungumzia juu ya mabadiliko juu ya kanisa – kurudia Ukristo wa Agano jipya, kurudia '***upendo wa kwanza'*** kwa '***kuyatenda matendo ya kwanza'"*** **Ufu.2:5**. Mungu anainua mitume wanaofahamu***"hekima ya Mungu aliyoiweka kabla ya vizazi kwa ajili ya utukufu wetu"*** **1Kor.2:7**; mitume na manabii wanao '***fahamu***' ***… siri, ambayo katika vizazi vingine hawakujulishwa wanadamu kama jinsi ambavyo imefunuliwa kwetu na Roho Wake kwa mitume wake watakatifu na manabii.'*** **Efe.3:4-5**. Vile Neno la bwana linavyozidi kufunuliwa katika mafundisho, bila kizuizi cha mafundisho ya kidini, mitindo na desturi; bila kutegemea wanadamu kuwadhibitisha, **Neno la Mungu linaendelea kukua na kushinda** (**Matendo19:20**). Haya ni yale yaliyotendeka Efeso wakati Paulo alipokaa huko miaka miwili, akifundisha kila siku katika shule ya Tirano (**Matendo19:9-10**) na kuhudumu nyumba kwa nyumba (**Matendo20:20**), matokeo yakawa Asia yote ikasikia Neno. Pia wahudumu wengi, yaani, watenda kazi, walifunzwa na Paulo.

LUKA ALIPOKEA UFAHAMU HAKIKA

Luka, aliyeandika **Injili** na **Matendo**, alikuwa mwanafunzi na mtenda kazi pamoja na Paulo. Alipata nafasi ya kukutana na mitume wale wengine ambao walikuwa na Yesu. Luka anatangaza katika **Lu.1:1-4,** kuwa anaweza ***"kuandika usahihi wa mambo hayo tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu*** (**a.3**) ***habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu"*** (**a.1**) [habari ya kuja kwa Yesu] ili Theofilo ***"upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa"*** **a.4**. Luka anasema kuwa

ana ***"usahihi wa mambo yote tangu mwanzo"*** **a.3**, yaani, **alifahamu siri kikamilifu kuhusu kuja kwa Yesu!** Amepokea ufahamu huu kutoka kwa ***"wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile Neno tokea mwanzo"*** **a.2**. Hili ni fundisho la mitume! Kanisa la kwanza 'liliachishwa maziwa' katika fundisho la mitume (**Matendo 2:42**).

MAARIFA YA UFUNUO WA MWANA WA MUNGU

Je, unajua kuwa ni rahisi kuwa na ufahamu mkamilifu juu ya kusudi la Mungu? Je, unajua kuwa ni kusudi alilotangaza Mungu kwako wewe? Paulo amatuombea katika **Efe.1:17-19**, kwamba ***"roho wa hekima na ufunuo katika kumfahamu Mwana wa Mungu Yesu Kristo."*** Na kwamba ufahamu wetu utiwe nuru. Mungu hakukusudia watu wake wafungiwe nje katika dini, wakifundishwa sehemu ya ukweli tu. Bali **Alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi, ili ateke mateka, na kupaa katika ulimwengu wa roho, na kuvijaza vitu vyote kwa kuwapa watu vip awa (Efe.4:8-9**). ***"Naye alito wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu."*** **Efe.4:11**. Huduma hizi zote sharti zifanye kazi ***"hata sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu makamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*** **v.12**. Wapendwa, hili litatendeka! Neno la Mungu limeamuru. Kanisa haliwezi kufikia utimilifu katika njia nyingine yo yote!

'UMOJA WA IMANI' **NI NINI?**

Ni ***"imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu"*** **Ju.3**. Nimesikia wahudumu wakuu wakiwa na shaka juu ya misingi ya mafunzo ya Neno la Mungu. Sasa tunachangamoto nyingi na kukana ***'imani'***. **Juda** anatutia moyo ***"kushindania"*** **imani**. Kwa maneno mengine **imani katika mafundisho ya mitume ambayo ndiyo maneno ya msingi ya ufunuo kuhusu ufalme wa Mungu na Bwana wetu Yesu Kristo**.

UKWELI UTASHINDA MAKOSA

Tusifanye mijadala na ukweli wa mafundisho ya Maandiko Matakatifu katika njia yo yote. Nimeona viongozi wakuu wakisimama na kuunga mkono washirika wa kanisa ambalo limejitangaza kuwa la uongo kwa kuwatawaza mabasha na walawiti katika huduma. **Hatustahi kusimama na udanganyifu wo wote bali tuukatae kwa bidii. Ni katika kukosa maarifa ya mafundisho ya mitume kiini cha kuwaacha wahudumu na wapendwa kunyimwa ukweli** kwa wakati wa muhimu kama sasa. Wanaoujua ukweli wanastahili kusimama bila mijadala na kuutangaza. Hii itagharimu na itakabiliana na upinzani wa aina yote na mateso.

POKEA MITUME AMBAO WAMETUMWA NA YESU

Paulo anatangaza katika **Efe.3** kwamba **Mungu amepeana neema ya ufunuo wa siri Yake kwa *"mitume wake watakatifu na manabii"* a.5**. Kanisa limenyimwa hii ***"hekima iliyofichwa"*** ya Neno la Mungu lakini sasa kwa sababu ya kurejeshwa kwao mitume na manabii, ***"siri, … ambayo Mungu aliazimu tangu milele kwa utukufu wetu"*** **1Kor.2:6-7**, inafunuliwa tena. Huduma tano za **Efe 4** alizotoa Yesu kuwakamilisha na kufanya kazi ya huduma, na kuujenga Mwili wa Kristo hadi sote tuufikie utimilifu. Huo utimilifu unaelezewa katika **aya ya 13-16**. Wakati mitume wanapojitokeza na kanisa liwapokee ndipo kanisa litapokea mafundisho na ufunuo unaohitajika kutusaidia kufikia utimilifu. Ukweli mwingi umethibitika katika siku za hivi karibuni, pamoja na wahudumu wengi waliopakwa mafuta wakitenda kazi hii.

Bali huu ndio wakati wa kupokea mitume ambao Yesu amechagu na kutuma.

WANA NA URITHI

Sehemu moja muhimu katika fundisho la mitume ni kufahamu jinsi ya kuwa Mwana, uhusiano wa Baba na Mwana, na kupokea urithi wa neema ya Mungu ambao tumewekewa. Ni ufunuo kuwa kanisa sio kikundi chenye mipango bali ni mwili ambao kwa karibu umeungamanishwa na kushikanishwa na upendo (**Efe.4:16**). Mungu ametoa neema ya kurejesha roho na uweza wa Eliya

kwa kanisa la nyakati za mwisho. Mungu aliahidi katika **Mal.4:5-6** kutuma **baba [mitume] walio na moyo kwa ajili ya wapendwa, moyo kwa ajili ya kanisa la Yesu Kristo,** na kupitia kwa neema hii **watakatifu watatambua roho wa Baba,** kufikia ukweli wa kuwa mwana, kushuhudia upendo wa Mungu katika njia ambayo inaleta ulinzi wa hakika na kusaidia kuendelea.

KUUNDA VIKUNDI VYA UTUME

120 KATIKA MATENDO 1-2, KIKUNDI CHA MITUME

Kikundi Cha Mitume kilianzia katika **Matendo 1**. Yesu alikuwa amewafundisha mitume na baada ya kufufuka aliwatokea mara nyingi akiwafundisha kuhusu ufalme wa Mungu. Aliwaambia wakae Yerusalemu mpaka wapokee Roho Mtakatifu. Baada ya Yesu Kupaa wale mitume kumi na mmoja pamoja na wanawake na mama wa Yesu na ndugu zake pia, kwa jumla 120, walikuja **pamoja katika chumba cha juu kwa umoja kwa maombi na dua, wakingojea kile Yesu aliwaahidi. Kikundi hiki kilijumuisha mitume ambao walikuwa wamechaguliwa na Yesu** [ila mmoja alikosekana], **wanafunzi** waume na wake pamoja na **jamaa wa Yesu ambao walikuwa wachanga kiroho.** Lakini walikuwa pamoja kwa umoja – na moyo mmoja na nia moja kutumikia makusudi ya Mungu, kumtii Yesu Kristo. Katika kungoja, Bwana alimnenea Petro kwa njia ya Maandiko kuhusu hitaji la muhimu la kujaza nafasi ya Yuda, msaliti maana walihitajikuwa kumi na wawili, mitume wa Mwana Kondoo. (**Ufu.21:14**).

ROHO MTAKATIFU ALISHUKIA KIKUNDI CHA UTUME

Ni kwa **hiki kikundi cha watu, katika mpangilio wa utume, kwa moyo mmoja na nia moja – pamoja, ndio Mungu alituma Roho Mtakatifu kuwezesha Kanisa kuzaliwa kikamilifu:**

Kwa kikundi kama hiki Roho mtakatifu alishukia
Kupitia kwa kikundi kama hiki makusudi ya Mungu yanatimizwa.

Siku hizi, Mungu ameweka katika mioyo yetu hamu Yake ya kuanzisha vikundi vya utume kwa mfano wa **Matendo 1**. Tayari ameinua mitume na anakusanya vikundi pamoja nao. Kwa miaka kadhaa, Mungu ameweka hamu na kunifunulia haja Yake na kusudi la kuunda vikundi vya watakatifu pamoja na mitume jinsi alivyofanya katika **Matendo 1**.

KUSUDI LA VIKUNDI VYA UTUME: kupokea Roho Mtakatifu

Mwaka wa 2001, nilikuwa nikimtafuta Bwana kuhusu kutimia kwa Sikukuu ya mabanda katika kanisa lililo hai na maisha ya Mkristo. Ufunuo ukaja kutoka kwa Bwana kutoka katika **Yoh. 7:37-39** ***"Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu alisimama, akapasa sauti yake akisema mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.' Na Neno hilo alinena kwa habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa."***

<u>Siku ya Mwisho, siku ile kubwa ya Sikukuu</u>

Aya ya 37 inasema kuwa Yesu alifanya tangazo la ajabu la kinabii kuhusu ***'siku ya mwisho'***, ***'siku ile kubwa ya sikukuu'***. Hii ni **Sikuku ya mabanda**. Mbeleni katika **Sura ya.7** wandugu wake Yesu walikuwa wamemuhimiza kujitokeza hadharani katika sherehe lakini Yesu alikataa. Hata hivyo alienda huko kwa siri na kuanza kuhubiri nje ya Hekalu. Maandiko yako wazi kuwa *'Siku ya mwisho'*, ambayo ilikuwa siku ya nane (**Walawi.23:36**); huu ndio wakati Yesu alisimama katikati yao na kupasa sauti.

Siku ya nane iliwadia baada ya siku saba za kusherekea Sikukuu ya Mabanda. Kidesturi na kimaandiko hii ilimaanisha watu wa Mungu walikaa katika mabanda yaliyotengenezwa na matawi ya miti na majani. Siku ya nane ilikuwa ya **kusanyiko maalum**, **kukuja pamoja**, **kusanyiko takatifu**, **siku maalum ya Sabato**. **Watu wote** waliokuja Yerusalemu kwa Sikukuu **walikusanyika** kwenye Hekalu '**kusongeza sadaka kwa moto'**. [Tazama **Walawi. 23** kwa

maelezo zaidi juu ya Sikukuu hiyo.] Wakati walipokusanyika kwa sherehe; **mwisho wa dahari itakuwa watakatifu wa kweli watamkusanyikia Yesu!** Yesu ataachilia Roho Mtakatifu juu ya waaminio kiwango kuwa wote walio na kiu watapewa kunywa.

Pasaka, Pentekoste na Mabanda

Israeli walipewa **Sikukuu muhimu tatu** na Bwana: **Pasaka**, **Pentekoste** [sikikuu ya majuma], na **Mabanda**.

Pasaka inajumuisha sehemu tatu: **Siku ya Pasaka**, siku saba za **Mkate Usiochachwa** na siku inayofuata, ni siku ya **Malimbuko**.

Pentekoste ilikuwa siku moja tu.

Mabanda pia ilikuwa na sehemu tatu: siku ya kwanza ya mwezi wa saba ilikuwa ya **'Kupiga Tarumbeta'**, **Siku ya Upatanisho**, na **Sikukuu ya Mabanda** yenyewe ambayo ilichukua siku nane. Siku ya kwanza ilikuwa Sabato Maalum na siku ya Nane ilikuwa Sabato Maalum.

Sikukuu zote zilikuwa za kutimiza jambo

Sikukuu zote zilikuwa za kinabii na **zinatimia ndani ya Kristo**. Pia kuna **timizo katika kanisa** la Yesu Kristo na hivyo **kutimia katika maisha ya kila mkristo**.

Kutimia kwa Pasaka

Hakika Yesu alikufa msalabani Siku ya Pasaka; Yeye akiwa timizo. Mwana Kondoo wa Pasaka alielekeza kwa Mwana Kondoo wa Mungu, Yesu. Tunaipokea Pasaka wakati ambapo tunakuja kwa Yesu kwa njia ya imani, tukijua kuwa ***"Alitolewa kwa ajili ya makosa yetu na kufufuliwa kwa ajili yetu kuhesabiwa haki."*** **Rum.4:25**. Mkate Usiochachwa ulisimamia kuondolewa dhambi juu yetu. Haya hutendeka wakati tunapookoka. Ubatizo wa maji ni kiungo muhimu katika wokovu na tunabatizwa katika ufufuo wa Yesu Kristo, (**1Pet.3:21-22**). Hili linatimiza Malimbuko: Yesu alikuwa wa kwanza kufufuka kutoka kwa wafu – Alikuwa 'Malimbuko' ya wale watakao fufuliwa kutoka kwa wafu.

Kutimia kwa Pentekoste

Sikukuu ya Majuma [Pentekoste] iliitwa hivyo kwa sababu ilikuwa ikisherehekea majuma saba na siku moja baada ya siku ya Malimbuko. Pentekoste ilitimia wakati Roho Mtakatifu Alipowashukia wale wanafunzi 120, pamoja na mitume, katika **Matendo 2:2-4**. Hii Sikukuu inatimia wakati mtu anapojazwa Roho Mtakatifu, pamoja na ishara na lugha.

Siku ya Upatanisho na Baragumu

Kitabu cha **Waebrania** kinaweka wazi kwamba Yesu Kristo alitimiza Siku ya Upatanisho kikamilifu kwa kufanyika *'Azazeli'* – Alienda nje ya mji kufa, akizibeba dhambi zetu; na kwa kufanyika *'mbuzi wa sadaka'* – Aliingia Patakatifu zaidi mbinguni juu na damu Yake Mwenyewe. Ku piga Tarumbeta hakujafafanuliwa kwa rahisi. Hata hivyo, tafsiri ya maana ni kuwa kupiga Tarumbeta kunawakilisha kutangaza kwa Neno la unabii la Mungu, kuliita kanisa katika utimilifu, kuandaa kanisa kwa ajili ya kurudi kwa Bwana.

Kutimia kwa Sikukuu ya Mabanda

Kuhusu kutimia kwa Sikukuu ya Mabanda, Yesu anatupatia ufunuo wa unabii katika **Yohana 7**. Alitoa tangazo hili siku ya Mwisho ya Sikukuu – siku ya nane. **Alikuwa akizungumzia juu ya kutimia kwa hii Sikukuu. Kuja kwa Roho Mtakatifu** siku ya Pentekoste ilikuwa ni kutimiza Sikukuu ya Majuma. Yesu hakuwa akizungumzia kuhusu kutimia kwa Sikukuu ya Pentekoste; Alizungumzia kutimia kulingana na **Matendo 1:4-8**. Katika **Yohana 7**, naamini Yesu anazungumzia Sikukuu ya Mabanda katika mwisho wa nyakati. Lakini hata kuja kwa Roho Mtakatifu Siku Ya Pentekoste ilikuwa ni **kuandaa watu** – wanafunzi120, kwa hivyo kuja kwa Roho Mtakatifu kufungua "vijito vya maji yaliyo hai" kutoka kwa waaminio ili walio na 'kiu' wanywe wale walioandaliwa. Kufikia hapo **Mungu anaunda vikundi vya utume** ulimwenguni

kote **ambao wataandaliwa na Mungu kupokea Roho Mtakatifu kwa ajili ya kutimiza Yohana 7:37-39** na

Kuleta kutimia kwa Sikukuu ya Mabanda katika uhai wa kanisa kabla ya kurudi kwa Yesu.

Roho Mtakatifu atashuka
Yesu atadhihirika miongoni mwa waaminio ambao wamempokea Yesu kikamilifu, wamekomaa ndani Yake ***"katika yote"*** (**Efe.4:15**), na wamekamilika, kanisa tukufu ambalo Analirudia (**Efe.5:27**). **Lakini kabla kurudi kwa Yesu kutakuwa na kushuka kwa Roho Mtakatifu kuwapa kinywaji walio na kiu, ili wengi waokolewe.** Sikukuu ya Mabanda ambayo pia inajulikana kama **Sikukuu ya kukusanyika**.

KUSUDI LA VIKUNDI VYA UTUME: kuonyesha mazoezi ya kanisa la Kimaandiko na kulitumikia kusudi la Mungu katika siku hizi
Katika siku hizi Kanisa kwa jumla linahitaji mabadiliko. Kanisa la kweli katika jumuia ni vigumu kulipata kulingana na Maandiko Matakatifu. Mengi ya yale ambayo kanisa lina simamia na kufanya hayalingani na Maandiko Matakatifu. Matendo ya kanisa ulimwenguni kote yanamsingi wake katika desturi za watu na kwa hivyo Neno la Mungu limefanywa kuwa halina maana. Mungu anaunda vikundi vya utume kulingana na maandiko Matakatifu kudhihirisha waaminio wa kweli, pamoja na wahudumu, waone dhihirisho, na utukufu wa Yesu Kristo miongoni mwa watu ambao wamejitolea kikamilifu kuwa Kanisa Lake. Watu wa aina hii wamewekwa kwa mpango, wako pamojana katika umoja na wengine, na wanatembea katika vipawa na huduma ambayo Kristo ametoa.

VIKUNDI VYA UTUME VINAUNDWA AJE SASA?
Mitume wanarejeshwa ili vikundi hivi viundwe. Wakati wote ambao Bwana anaainua mtume, **Anawainua wengine kusimama na huyo mtume**. Katika ujuzi wa huduma yetu, kuna watu waliojitolea na kukubali kuweka msingi wa huduma hii katika kutii ufunuo ambao tulikuwa nao. Tulijua kuwa Mungu alikuwa anatuita kuwa huduma ya utume lakini hatukujua tutafanya nini. Kile kilichokuwa wazi ni mshikamano katika Maombi na uvuvio na ujasiri kuwa Mungu atatuongoza. Karibu miaka mitano tulifanya kazi pamoja na wapendwa waliojiunga pamoja nasi na kuhudumu nasi. Mbeleni tulijiona kuwa **kikundi cha utume cha kuomba na kusaidia**. Bwana alituonyesha kufundisha jinsi ya **kuanzisha vikundi vya utume** na tukawaalika **wapendwa ambao walikuwa na makubaliano nasi** kuhusu mapenzi ya Mungu kwa ajili yetu kujiunga na kikundi kama hicho.

Kwa kujiunga na kikundi cha utume wapendwa **wanarudi kwenye mpango** kama vile imedhihirika katika kitabu cha **Matendo**. Kwa kujiunga na kikundi cha utume **kuna leta kuhudumu katika vipawa na huduma kwa uhuru**. Watu wanaoishi katika maeneo yasiyokuwa na mtume wa kuhusiana naye wanaweza kujiunga na kikundi cha utume na hivyo kupokea uangalizi, kuungwa mkono na kulishwa chakula wanachohitaji kuwawezesha **kukua na kujiendelea katika maeneo ya mwito wao**. Kunakuwa na hali ya kuwa nyumbani na ulinzi; kitu ambacho watu wengi hukosa – sio ulinzi kwa sababu ya kuchungwa vizuri na mchuungaji bali **ulinzi kuwa umejiunga na kikundi cha waaminio ambapo kila mtu alipokelewa na kukubaliwa** kama kiungo muhimu katika mwili.

Viriba vipya
Ilikuwa baada ya miaka tano ya kujijenga na kuendelea katika huduma ya utume na baada ya miaka miwili ya kutafuta kuanza kikundi cha utume, ndipo **tulikuja katika uhusiano na mtume mwingine na neema ya kufanyika wana ikaja juu yetu. Ukweli wa ufahamu wa wa kufanyika wana uhusiano wa baba kufanyika viriba vipya vya kanisa** kumeendelea kuongezeka juu ya kuwa katika kikundi cha utume. **Kuna uhakika wa kuwa katika jamii, maongezeko ya upendo na kuaminiana, ambapo wandugu wanasikia kuwana ulinzi, ujasiri, nidhamu, na kujua eneo lako na kazi katika mwili. Tunabarikiwa kuwa Baraka! Tunaufunuo kuwa neema ya Mungu**

inatosha na kwamba urejesho wa mitume ambao ni ulimwenguni kote katika kanisa la Yesu Kristo hautazuilika!

KIKUNDI CHA UTUME KINACHOFANYA KAZI

Mara tu kikundi cha utume kinapoanza kufanya kazi, yaani, kufunza na kujenga watenda kazi kwa ajili ya mavuno, na kudhihirisha kanisa la Agano Jipya, tutaona watenda kazi wakiingia katika mavuno na makanisa mengi kupandwa. Mara makanisa yanapopandwa, mtume au mmoja katika kikundi cha utume atakuwa mwangalizi wa kuwakuza watenda kazi, wazee wawe waangalizi na wachungaji wa kundi la Mungu ambao wanakutana katika nyumba.

SURA YA SITA

KUJENGA KANISA
- kituo cha mafunzo ya utume
- kupanda makanisa mengi

KUZA WATENDA KAZI KWA AJILI YA MAVUNO

Ufunguo wa kujenga kanisa ni kukuza watenda kazi wengi kwa ajili ya mavuno. Yesu katika **Matt.9:37-38** na **Lu.10:2**, alizungumzia mavuno kuwa mengi na kuna haja ya watenda kazi kupelekwa na Bwana wa mavuno. Baada ya kusema haya katika **Mathayo,** Yesu **aliwachagua mitume kumi na wawili** na kuwatuma katika mavuno, huku akiwapa mamlaka ya kuhubiri na uwezo wa kuponya. Vivyo hivyo katika **Luka**, Yesu **aliwachagua wengine sabini na kuwatuma katika mavuno** kuponya na kuhubiri. Yesu alisema katika **Mathayo 16:18,** ***"Nitalijenga kanisa langu"*** na kwa kukuza wale kumi na wawili na wale sabini Yesu anatuonyesha jinsi ya kujenga kanisa:

Funza watenda kazi na uwatume na uwezo wa kuponya na kutoa pepo wachafu,
Mamlaka ya kuhubiri ufalme wa Mungu.

Baada ya kupaa Kwake, Yesu alitoa huduma tano na akazipeana kwa kanisa (**Efe.4:11**) na tunatakikana **kuufuata huu mfano ambao Yeye aliithinisha**: kuza watenda kazi na kuwatuma katika mavuno na kupanda makanisa. **Paulo mtume aliufuata mfano huo na akaweza kwa bidii kuyapanda makanisa mengi, baada ya kukuza watenda kazi wengi na kisha kutawaza wazee kila mahali.**

KITUO CHA MAFUNZO YA UTUME

Shule ya mafunzo ya Yesu kwa mitume na watenda kazi wengine ilikuwa ya kuhama hama – aliwafundisha huku wakimufwata. Kumbuka alipowaita baadhi ya wanafunzi aliwaambia, ***"Nifwateni nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu."*** Aliwafundisha wanafunzi wakiwa wanaishi Naye, wakisafiri Naye, walipojifunza kuomba Naye, walimuona akihudumu katika nguvu za Roho, na walimsikia akihubiri na kufundisha Neno la Mungu. Pia aliwatuma na nguvu za kuhubiri na kuponya. Wanafunzi hawa walikuwa na Yesu kila mahali katika 'kufunzwa ukiwa kazini' muundo wa mafunzo ambao ulichukuwa karibu miaka mitatu na nusu. Hii ni tofauti na shule nyingi za Biblia katika historia ya kanisa na matendo ya kisasa. Bali katika historia ya kanisa tunapata ushahidi wa matendo ya utume.

MITUME KATIKA HISTORIA

Katika karne ya kumi na mbili kulikuwa na mtume kwa jina Peter Waldo ambaye alikuwa mmoja wa mitume wengi ambao wakati huo walikuwa **waangalizi wa upanzi wa makanisa na kukua kwa makanisa mengi kwa namna ya makanisa ya Agano Jipya** katika maeneo ya Ulaya. Mitume wa wakati huo walikuwa wa kuhama hama, **'wakipanda na kunyunyizia maji'** na wakati wote wakiwa na **msaidizi mchanga ambaye alikuwa katika mafunzo katika huduma ya utume, akisafiri na mtume mkuu**. Makanisa ya kila mahali, kama yale ya nyumba kwa nyumba, yalichungwa na wazee ambao waliteuliwa na mitume. Ni jambo la kuhuzunisha kutambua kuwa wapendwa hawa walipingwa vikali na kuteswa na watu wa kanisa la nyakati hizo, ambao ni wa kanisa la kikatuliki. Hakika katika historia ya kanisa kumekuwa na hadithi inayoendelea ya Ukristo wa kimitume ambao ulivuma kwa kuleta mazao katika kila mji na vijiji. Hata hivyo, makanisa tawala katika miji hiyo kila wakati yalitafuta kunyamazisha, kugandamiza na mara nyingi kuwaua viongozi wa kimitume na wapendwa wengi.

SHULE YA TIRANO – CHUO CHA SHULE YA UTUME

Baadaye mtume Paulo alianzisha shule kule Efeso na alikuwa huko kwa muda wa miaka miwili. Alifundisha kila siku katika shule na pia kuhudumu nyumba kwa nyumba. Hakuondoka mjini. **Matokeo yakawa kuwa watenda kazi wengi waliandaliwa kwa ajili ya mavuno.** Hata kwa kipindi hicho cha miaka miwili ***"wote waliokaa Asia walisikia Neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani."*** **Matendo19:10**. Watenda kazi walipotoka shuleni wakiwa na nguvu za kuhubiri na kuponya! **Huu ndio mfano wa shule za utume leo.** Paulo alimtarajia Timotheo kufanya jinsi yeye alivyofanya: ***"Na mambo ambayo umeyasikia kutoka kwangu mbele ya mashahidi wengi*** [katika shule ya Tirano] ***wakabidhi watu waliowaaminifu, watakaofundisha wengine pia"*** **2Tim.2:2**. Paulo kama mtume alifanya kazi ya huduma kama mtume, yaani, kuwakuza wahudumu wengi wa injili. Kisha akamuagiza Timotheo, ambaye alikuwa amefanyika mtume pia, kuifanya kazi ya utume: kukabidhi mafundisho kwa ***'watu waliowaaminifu, watakaofundisha wengine pia.'*** Leo hii moja wapo ya huduma kuu ya mitume ni kuwafundisha wengine kwa ajili ya kazi ya huduma. Kufikia hapo, shule za mafundisho ya mitume zinatakikana kufunguliwa.

ISHARA NA MAAJABU NI SEHEMU YA MAFUNZO

Tambua kuwa ***"Mungu akafanya kwa mikono ya Paulo miujiza ya kupita kawaida"*** **Matendo19:11-17**. Hili ni katika misingi ya shule za utume! Tena jinsi ilivyotofauti na shule nyingi za Biblia za leo ambazo zinasisitiza masomo na mawazo. Wanafunzi katika shule za utume wanafundishwa Neno, hata siri zilizofichwa za Neno, **1Kor.2:6-7**, na wanajengwa jinsi ya kuhudumu katika Nguvu za Mungu. Alama moja ya mtume ni kwamba huduma yake inakamilika kwa ***"ishara na ajabu nyingi na matendo makuu"*** **2 Kor.12:12**.

WANAFUNZI WALISAFIRI NA PAULO

Baadhi ya wale waliokuwa wakifundishwa na Paulo **pia walisafiri naye alipokuwa akihama hama kama mtume**, alikaa Efeso kwa muda wa miaka miwili akiwa mkaazi kwa muda mrefu zaidi mahali pamoja. Kama ilivyokuwa na Yesu ndivyo ilivyokuwa na Paulo mtume. Wahudumu wa siku za usoni pamoja na mitume wanafundishwa wakifanya kazi, wakiongozwa na mtume mwenye ujuzi na kikundi cha utume.

MTUME NI KIELELEZO

Paulo alitarajia wahuduma wale ambao alikuwa akifundisha na wapendwa katika makanisa mbali mbali ambao alileta kwa Bwana katika injili, kuuiga mfano wake (**Fil.3:17**), kumuiga Paulo. Aliwahakikishia Wakorintho kuwa Timotheo ***"atawakumbusha njia zangu katika Kristo, jinsi ninavyofundisha kila mahali"*** **1Kor.4:17**. Mitume wote ambao Yesu alifundisha na wale Paulo alifunza, waliufwata mfano wa shule za utume ambazo Yesu alianzisha. Hii ndio imekuwa njia inayofaa ya kulijenga kanisa.

KUUFWATA MFANO LEO

Mzigo wa Bwana moyoni mwangu tangu kuanzishwa kwa Huduma ya Uvuvio ya Australia umakuwa **wa kuwakuza watenda kazi kuingia katika shamba la mavuno**. Hili lilithibitika kwangu baada ya kusoma kitabu chake Rick Joyner, *'World Aflame'* mapema 1998. Rick ananukuu kuwa mojawapo wa sababu ya kuisha kwa haraka kwa uvuvio wa Wales ni **ukosefu wa watenda kazi walikuwa wamefundishwa kuchunga na kufanya wanafunzi wale maelfu waliookoka.** Wengi wao waliokoka kutoka kwenye mikutano ya uvuvio ambayo haikuwa na uhusiano na makanisa ya mahali. Tulipoanzisha huduma ya Uvuvio ya Australia tulijitolea kwa uvuvio wa Australia na bado tumejitolea. Lakini kwa miaka sasa, Bwana ametuleta katika huduma ya Utume. **Tumekusudia kumuomba Bwana kwa ajili ya watenda kazi.** Bwana anapotupatia watenda kazi, **tunawafundisha, kulingana na hitaji, na kuwatuma kwenda kufanya kazi.** Tulipoandika msingi wa mpango wetu mapema 1998 ambao ulikuwa msingi wa muelekeo wa huduma yetu, tuliufananisha na mfano wa Paulo wa kuanzisha shule za utume katika **Matendo 19** katika Efeso.

MFANO WA MYANMAR

Februari 1999, nilitembelea nchi ya Myanmar [iliyoitwa Burma] na kumtumikia rafiki yangu ambaye ni mtume katika taifa hilo. Kwa miaka mingi amekuwa akiwafundisha wanafunzi katika hiyo nchi na kuwatuma kuhudumu. Matokeo yamekuwa uinjilisti na upanzi wa makanisa mengi katika nyumba. Shule za mafunzo ya mda mfupi yamefanyika mara mbili kwa mwaka katika sehemu mbali mbali katika hilo taifa. Nilifanikiwa kuhudumu katika moja ya hizo shule kwa siku chache [karibu wanafunzi 120 ambao walikuwa wakijifunza kwa muda wa majuma sita] halafu nikasafiri kaskazini nikiwatembelea wandugu katika miji mingi. Walikuja pamoja katika mikutano ya nyumba ambapo ningefundisha na nguvu za Roho Mtakatifu zilikuwa dhahiri. Nilishuhudia

Kanisa la Agano Jipya katika matendo:
Shule ya mafunzo ya utume na kanisa la nyumba katika kila mji

MFANO KATIKA MATENDO

Mungu alinionyesha wazi kupitia kwa ndugu mtume huko Burma mfano katika matendo. **Tulifanya mkutano wetu wa muhula wa kwanza** mwezi wa sita na wa saba mwaka huo Australia, **na kuanza kupanda makanisa ya nyumba**. Tangu wakati huo tumekuwa tukifanya shule mara mbili kwa mwaka hapa Toowoomba. Hivi sasa shule zetu zinafanyika majuma mawili mfululizo; pia, shule za juma moja zimekuwa zikiendeshwa katika miji mingine na ng'ambo. Shule zimefunguliwa lakini zinalenga sana wachungaji na wahudumu wengine na viongozi, na wanafunzi ambao wamejitolea, ambao wanataka kujifundisha na kujengwa. **Wengine wao wametawazwa** katika moja ya huduma tano za Efeso 4 baada ya mafunzo. **Wote wanaomaliza shule hutumwa** kwa kuwekewa mikono. **Huduma zingine zinapokewa katika kufundisha** katika shule. Tumekuwa na mitume, manabii, na waalimu hata wainjilisti huja kushiriki wakati ambapo tunapokea kila huduma ambayo imetumwa na Yesu, na tunabarikiwa.

SHULE YA UTUME YA UANAFUNZI YA SHILOH

Shule inaorodhesha utumizi wa vitabu vya mwongozo* ambazo tayari imeandikwa; fundisho ambao ni ufunuo mpya na ufahamu kutoka kwa maandiko ambao utaunda kitabu kipya cha mwongozo; kufunzwa maombi, katika uinjilisti, katika huduma, katika utafiti wa Biblia, na mazoezi ya kuhubiri. Huwa tunawafunza watoto katika shule ya uanafunzi kwenye huduma nyingine kando yake, inayoenendelea sambamba na shule ya watu wazima. Shule hizi ni nafasi yakuwa katika ushirika wa kikundi wa kitume na kuhisi wazi wazi kazi ya Mungu ikidhihirika miongoni mwetu.
*[vitabu vya mwongozo vimeandikwa kwa sababu ya kufanya uanafunzi na kwa kusudi la kimasomo

HATUA SABA ZENYE KULETA MATOKEO MAZURI KATIKA KUTIMIZA UTUME MKUU KWA KUPANDA MAKANISA YA AGANO JIPYA

Tunawatayarisha wafanyi kazi kwa mavuno. Wafanyi kazi katika mavuno sio tu wainjilisti na wavuna nafsi, ingawa tunasisitiza uinjilisti. Hata hivyo huduma yetu ni ya kitume kwa hivyo sisitizo letu ni kupanda makanisa mengi kuzidisha. Kuna kiolezo wazi kwetu kwenye maandiko sisi kufuata katika kulipanda kanisa.

Hatua hizo saba ni:

1. **MAOMBI** na
2. **UINJILISTI** > ambayo kwa **kanisa hupandwa**

3. **MAFUNZO** na
4. **UANAFUNZI** > ambazo kwazo **kanisa hukua na kunawiri**
5. **KUELEKEZA na KUANDAA kwa HUDUMA,** na

6. **KUPANDA KANISA** na
7. **KUINUKA kwa HUDUMA ZIPYA** >ambazo kwazo **kanisa huletwa kwa ukomavu.**

[Kwa masomo Zaidi na kutumia hatua hizi, angalia vitabu vya mwongozo: 'Mbinu za kufikia Taifa' na 'Kupanda Kanisa']

MAOMBI NA UINJILISTI

Kanisa linapandwa kwanza kupitia maombi: waumini wawili au watatu kuja pamoja kwa kukubaliana katika maombi kwa waliopotea, kwenye mahali ambako wanaishi, au mahali ambapo Bwana amewatuma kupanda kanisa. **Kutoka kwa maombi, Bwana hutembea na nafsi hufikiwa na kuokolewa.** Kuna shuhuda za nguvu za watu kuvutwa kuokolewa lakini mara nyingi Zaidi, **majirani kwa urahisi hukubali mwaliko wa kuja kwenye nyumba** kwa mlo na kuanza kusikia Injili. Katika mojawapo ya miji ya nchi yetu ambapo huwa tunahudumu mara kwa mara katika kanisa la nyumbani, watakatifu wengi kutoka makanisa mbalimbali walikuwa wakikutana kusikiliza fundisho la mitume. Hata hivyo hivi majuzi, hao kwa jumla wameacha kuja na badala yake nyumba imejaa kina mama na watoto kutoka kwa mtaa uo huo.

Majirani wameafikiwa na kuguzwa na imani ya mume na mke wenyeji na sasa wao huja na watoto wao, kujumuisha vijana.

Makanisa ya nyumbani ya kweli

Tuna shuhuda za makasa mengine ya nyumbani ambayo yanafanya kazi kulingana na kielezo cha Andiko na kuzaa matunda.

Hii ni mifano ya kweli ya huduma katika nyumba kulingana na Matendo 2:42-47: mtume anakuja kufundisha; kuna ishara na miujiza mara kwa mara; waumini wako pamoja, wakisaidiana, wakila pamoja, kuumega mkate na mume na mke wenyeji wana kibali na mji wao wote au wilaya. Kwa hivyo Bwana anaongezea kwa kanisa wale ambao wanaokolewa.

KANISA KWENYE NYUMBA

Tunapaswa kuwa wazi:
Kanisa la Agano Jipya pasipo kuchanganya lilipandwa kwenye nyumba.
Yote yaliyo sehemu ya kanisa katika Agano Jipya ni wazi kwamba yameidhinishwa na neno la Mungu kufanya kazi kwenye makanisa ya nyumbani.

Wokovu hufanyika kwa nyumba, **kujumuisha ubatizo kwa maji.** Kama hakuna bwawa karibu au mto wa maji, bakuli za kuogea zinaweza kuwa mbadala bora. Ubatizo haiwi na nguvu kwa sababu imefanywa kwenye jengo la kanisa lililowekwa wakfu au kwa sababu ibaada maalum ya ubatizo imepangwa baada ya kila miezi michache na kanisa la kirasmi na mhudumu aliyewekwa wakfu akiwepo. Ubatizo, kulingana na neno la Mungu, una nguvu kwa sababu **ni ubatizo ndani ya Kristo, ndani ya jina la Mungu la nafsi tatu za Mungu kwa moja, katika jina la Bwana Yesu Kristo.** Maombi ndiyo ufunguo kwa kupanda kanisa, kuwavuta waliopotea mahali popote pale.

WAINJILISTI NA MITUME

Wainjilisti wanaweza kutumwa mahali ambapo matayarisho ya maombi 'yamevunja na kufungua ardhi'.Kutuma muinjilisti kwenye sehemu ambapo hapana msingi wa kanisa kuaweza kuwa na kutozaa matunda hatimaye.Hatahivyo,**muinjlisti akienda mbele ya kikundi cha kitume,**basi,kama vile Samaria katika **Matendo 8,**mitume wanaweza kuweka msingi vizuri kwa kanisa hilo jipya.Kwa sasa katika baadhi ya mataifa ya Kafrika,mikutano ya umati hufanywa na maelfu ya maamuzi hurekodiwa kwa Kristo lakini sio wengi wa 'waliobadilishwa' hubatizwa na hata ni wachache wanaolelewa na kufanyiwa uanafunzi katika kanisa la mahali pale [yaani,kanisa la nyumbani].

Wainjilisti wanahitaji kufanya kazi na mitume ili kwamba kanisa liweze kuumbwa vizuri.

KULIWEKA KANISA MSINGI VIZURI

Hata hivyo mahali kanisa la kitume tayari limeanzisha na kutayarisha wafanyi kazi si tu kwa '**mashauri ya wokovu'** bali kwa **kuwalea na kuwafanya wanafunzi waumini wapya,kanisa linaweza kuzidishwa kwa vile wengi wanaokolewa.**Wainjilisti wanahitaji kuhubiri **Injili ya ufalme wa Mungu,**na si injili ya 'wokovu',ambayo **haijumuishi ubatizo wa maji** au **kupokea Roho Mtakatifu.**Wainjilisti wanahitaji kufanya pamoja na mitume ambao wana jukumu la kujenga kanisa;kisha kanisa linaweza kuchipuka kila mahali,na misingi ya nguvu ya kibibilia.

KULEA NA KUFANYA UANAFUNZI KUKUZA KANISA

Kukuza kanisa inahusisha kulea na kuwafanya wanafunzi kuwa waumini wapya, ili waweze kukua kufikia ukomavu, kuwezeshwa kuenenda na kuhudumu katika mwili mpana Zaidi wa Kristo. Huduma ya mchungaji/mwalimu husimamia makanisa ya nyumbani,kuchunga kundi la Mungu,kulingana na Paulo katika **Matendo 20:28** na Petro katika **1Pet.5:2-4.**Waumini wapya mara nyingi huwa na mahitaji ya ndani na wanahitaji huduma ya uponyaji na urejesho.Ili kuafikia haya mahitaji,makanisa tofauti ya nyumbani yanaweza kuja pamoja kila baada ya miezi michache na kualika huduma ya uponyaji kuja kuwahudumia waumini wapya.Malezi kimsingi ni kuwalisha wale wapya ***"maziwa ya neno ili waweze kukua"*** **1Pet.2:2,**kuwafundisha mafundisho ya kimsingi ya Kristo kama yalivyowekwa katika **Waebrania 6:1-2.**

Tunawafanya wanafunzi waumini kwa kuwafundisha, neno la Mungu, kuwahimiza wote kwenye nidhamu ya kusoma Maandiko. Mwanafunzi ni yule anayefundishwa-wanafunzi wanahitaji mwalimu. wanafunzi ni wale ambao wanajifunza kumfuata Bwana, kuwa kufundishwa katika neno, ili waweze kuwa na nguvu, kumshinda yule mwovu.

Malezi na uanafunzi ni jukumu la mchungaji/walimu
Na hufanyika katika maisha ya kila siku ya kanisa.

Kusoma Maandiko kwa nidhamu

Katika jamii yetu,SHILOH,sote tumekuwa tukisoma Agano Jipya kwa msingi wa kujitoa wa **sura tatu kila siku.**Tumeunda mipango ya kila mwezi,kwa hivyo wote wana chapisho cha mpangilio cha kusoma[inachukua takriban miezi mitatu kusoma Agano Jipya].Ni furaha kuwa katika mojawapo ya nyumba za jamii na kuona vijana waume na wake wakichukua wakati mwisho wa wiki wakisoma Maandiko kwa bidii; kuwasikia wakisema wanaamua kwa maksudi kukesha usiku moja kwa wiki kufikia lengo lao katika mpango wa kusoma.**Ufunguo wa uanafunzi ni kuwafanya wanafunzi waumini wote katika kujitoa kwa sharti kusoma na kuijaza moyoni Neno la Mungu.**Ni mshangao kwangu kupata waumini wengi katika makanisa mengi hawawezi kusema wamesoma Bibilia yote.

KUENDELEA KUFIKIA UKOMAVU

KUTAYARISHA NA KUANDAA WATAKATIFU KWA HUDUMA

Mara mwumini anapofanywa mwanafunzi anakuwa tayari kutayarishwa na kuandaliwa kwa huduma. Hii kwa jumla haifanyiki katika makanisa ya nyumbani; hi ni kazi ya huduma ya mtume; hii ndiyo sababu tunahitaji shule za huduma za kitume na nafasi ya wanaotayarishwa kusafiri katika kundi pamoja na mitume kwa matayarisho zaidi.

KUPANDA MAKANISA MAPYA

Mara mwanafunzi anapotayarishwa, au mhudumu anapotayarishwa tena,hao ndio wanaweza kupanda kanisa.**Kumbuka kanisa lina pandwa katika nyumba iliyo na urafiki.** Katika **Matendo 16,**mara Lidia alipopokea neno la Bwana kupitia kwa Paulo na kubatizwa, aliwakaribisha kundi la kitume kupanda kanisa katika nyumba yake. Baadaye katika **Matendo16,** Huduma ya maana ilifanyika katika nyumba ya askari jela wa Filipi.Katika **Luka 10** Yesu alisema, '**Tafuta mtu wa Amani, kaa katika nyumba yake na kuhudumu pale-waponye wagonjwa na kuhubiri ufalme**

wa Mungu'. Watu wataokolewa! Kanisa litaanza! Wabatize waumini wapya haraka iwezekanavyo-katika Maandiko hiyo ilikuwa mara. Ubatizo ni sehemu kiini cha wokovu, si kitu cha kufanywa baadaye.

KUCHIPUKA KWA HUDUMA ZIPYA

Wafanyi kazi waliotayarishwa wanapoanza kufanya kazi katika huduma, kupanda makanisa mapya, kuhubiri, kufundisha na kuponya, upako na vipawa ambavyo Mungu ameweka ndani yao vitaonekana. **Kizazi kipya cha wahudumu na watakatifu walio na vipawa kitachipuka.** Itakuwa wazi kuona nani ni mtume mchanga, nabii anayechipuka; muinjilisti atajulikana kwa kipawa kujidhihirisha-wengine wanazaa matunda sana katika kushinda hali ya kawaida kwa sababu wana kipawa. Mchungaji atatambulika
Na waumini wengine watachipuka na vipawa vya uponyaji, wengine na huduma ya ukarimu, n.k.

Miaka mengine ya nyuma, kikundi cha waumini waliongozwa kutoka kwa kanisa la kidini na katika mapenzi ya Bwana wakaanzisha kanisa la nyumbani, ambalo lilipokea huduma yetu ya kitume. Mmoja ya ndugu hao kwa haraka akachipuka kama mchungaji wa kanisa hili, si kwa sababu aliteuliwa na binadamu, bali kwa sababu **'alichunga kundi la Mungu',** kwa kipawa cha Mungu - ana kipawa cha kupaa cha huduma ya mchungaji **(Waefeso 4:11).** Baadaye tulimweka wakfu huyu ndugu na anajulikana kama mchungaji.

UHUSIANO KATI YA WAZEE NA MITUME

KIOLEZO CHA MAANDIKO

Hiki ndicho kiolezo cha Maandiko: mtume anapanda kanisa katika mji au jiji au kijiji,au kanisa linaanza kwa njia kuu,na baadaye **'wazee [mchungaji/mwalimu] wanawekwa wakfu na mtume' Matendo 14:23.** Makanisa mengi leo hayajapandwa na mitume lakini katika mabadiliko ya kanisa, **kila mchungaji na kila kiongozi wa huduma anahitaji kuja kwa uhusiano na mtume kama mshauri/baba wa kiroho.**

VIWANGO VIWILI VYA UTAWALA

Katika Agano Jipya kuna **viwango viwili vya utawala ambavyo Mungu ameweka katika Mwili wa Kristo:**

utawala wa kanisa kwa jumla ni jukumu la mitume;
utawala wa kanisa la mahali ni jukumu la wazee.

Kuchipuka kwa kikundi cha kitume

Katika siku hizi za urejesho, **mabadiliko ya kanisa** yanaanza kufanyika. Kama vile Mungu ametuweka kwenye kikundi cha kitume, tumeshuhudia **kuchipuka kwa kikundi cha kitume, yaani, mtume na wale walioitwa na kupewa vipawa kufanya na mtume katika huduma ya kitume na kinabii.**

Kikundi hiki:

hufanya kazi ya huduma ya mtume
hufanya kazi ya huduma ya nabii
huenda kwa taifa na mataifa;
husimamia huduma, wachungaji na shirika
huhudumu katika shule za matayarisho ya kitume
na ni kwa kikundi hiki ambako ndugu huhusiana katika
uana wa kiroho.

Kuchipuka kwa wazee

Pia tumeshuhudia **kuchipuka kwa wazee, yaani, mchungaji/mwalimu** ambao

wanajukumu kwa makansa ya mahali ambayo yanakua katika idadi ya nyumba.

Wazee husimamia shirika za mahali;
wazee ndio wachungaji ambao wanachunga kundi la Mungu;
wazee ndio walimu ambao hulisha neno la Mungu kwa watu;
wazee wamewekwa wakfu na hivyo kutambuliwa na kupokelewa na mtume
wazee huhusiana na mtume au wanachama wa kikundi cha kitume.

MWISHO

KUJA NYUMBANI

Neema ya kitume inapoendelea kuachiliwa zaidi na zaidi kwa watakatifu, wengi wanapata uzoefu wa 'kuja nyumbani'. Kuna hisia ya kweli ya **kutoka kwa safari ya jangwa** na **kupata mahali pa kweli pa pumziko ndani ya Kristo.** Hii inaweza kufahamika kwa lugha ya Maandiko kama ***'kuja kwenye nchi',*** kama kuja kwenye ***'utimizo wa Sherehe ya Mabanda',*** kama ***'kuingia ndani ya pazia kwenye Patakatifu pa Patakatifu'.*** **In atiliwa mwisho na Mungu kwenye kundi la kitume;** ni **kuja kujua baba wako wa kiroho** na **kupata usalama wa upendo, kukubaliwa na kuidhinishwa.**

KUPOKEA URITHI WETU

Sasa tumo katika nafasi ya kupokea urithi wetu,
Kufundisha mafunzo ya kweli,
Kuiga mfano wa mitume ambao ulianzishwa na Yesu na wale kumi na wawili halafu baadaye Paulo.
Dhawabu na Baraka zitatiririka kwetu, tunapoanza kutii amri za Yesu na Neno la Mungu.

Kama vile Mungu anavyowaahidi baraka nyingi wanaotoa zaka zao katika **Mal.3:10-12**, ndivyo tulivyo na baraka nyingi wakati ambapo tunafwata matendo ya Agano Jipya katika uinjilisti ambapo ubatizo ni wa muhimu na wandugu wanapokea Roho Mtakatifu. **Siku inakuja ambapo wote wanaosikia mahubiri ya Neno na kushawishika wataokoka katika njia ile ya wale 3000 siku ya Pentekoste na kuongezeka kwa kanisa.** Hatutazumgumzia tena kuhusu 'asilimia' ya wale wanaofanya uamuzi katika mikutano ya hadhara ambao hujiunga na kanisa.

KUDUMU

Tunapo mega mkate mara kwa mara nyumba kwa nyumba na kupanda kanisa katika kila nyumba tunayoalikwa, tutaanza kuona anga mpya ya kanisa – kila siku, nyumba kwa nyumba. Yesu anatuahidi katika **Matt.10:40** kwamba tukiwapokea mitume aliowatuma tunampokea Yeye. **Tunapodumu katika fundisho la mitume, tutaendelea kukua katika ufunuo wa ufahamu wa Yesu Kristo.** Waaminio wa kweli wana njaa ya hekima iliyofichwa na Yesu na katika **Ufu.2:4-5**, Yesu anatwambia tutubu kwa sababu '***tumeacha upendo wa kwanza***'. Tunapofanya ***'matendo ya kwanza'*** tutautambua ***'upendo wa kwanza',*** kwa Yesu.

Kanisa linapobadilika na kuendelea kudumu katika matendo ya kwanza,
Kuingia katika mpango wakweli
na kutembea katika vipawa na huduma ya Agano Jipya,

kanisa la Yesu Kristo litajengwa
kulingana na mfano wa Maandiko Matakatifu
jinsi ilivyokuwa mwanzo.

Kama ilivyoandikwa.

"Yesu mwenyewe analitakasa na kulisafisha kanisa kwa maji katika Neno apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lo lote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa." **Efe.5:26-27**